**Bunge** laishukia halmashauri mkopo bil. 1.5/-

UKURASA 5


**Gwajima** aonya watoto kulala na simu

UKURASA 8



**Wajua** kwa nini ndoa nyingi zinavunjika?

UKURASA 11





UKURASA 9

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Februari 11, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581583
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# CHUMA KIMELALA

**SABABU** ya kifo yatajwa, Rais Samia, Kikwete wamlilia ...

*Endelea ukurasa. 2 & 3*



## DK. ZEPHANIA KAMEETA

# Askofu, mwanaharakati, waziri aliyepita milima na mabonde



UKURASA 4

MICHEZO NIGERIA, IVORY COAST FAINALI NZITO AFCON UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# HATIMAYE CHUMA KIMELALA



Waziri Mkuu mstaafu, Edward Ngoyai Lowassa akiwa katika moja ya mikutano yake ya kisiasa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), enzi za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

**Na Waandishi Wetu**

CHUMA kimelala. Kauli hiyo ndivyo inavyosadifu na tukio kubwa la kisiasa lililoitikisa Tanzania kutokana na kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania na mbunge wa zamani wa Monduli, Edward Lowassa.

Lowassa anaweza kuitwa chuma kutokana na enzi za uhai wake, akiwa kiongozi wa juu serikalini na hata alipoondoka madarakani, alivyotikisa katika medali za siasa. Hayo yalijidhihirisha alipokuwa Waziri katika serikali ya awamu ya pili na ya tatu kabla ya kuwa Waziri Mkuu serikali ya awamu ya nne.

Katika serikali ya awamu ya pili chini ya Rais (mstaafu) Ali Hassan Mwinyi (1990 hadi 1995), Lowassa alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na baadaye Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Katika nyadhifa hizo Lowassa alionyesha uwezo mkubwa katika kuzimudu. Katika Wizara ya Ardhi, kwa mfano, aliongoza opersheni dhidi ya waliokuwa na viwanja pamoja na mashamba bila kuviendeleza huku baadhi wakipokwa kwa kuviacha vichaka na mapori.

Wakati wa serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa, Lowassa alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira kabla ya kuwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo. Aling'ara zaidi katika wizara ya maji baada ya kufanya ziara karibu nchi nzima kufuatilia utendaji katika sekta husika. Hakika kila alikokwenda hakuwa mtu wa mzaha. Penye upungufu alikuwa akitoa maagizo bila kumung'unya maneno.

Baada ya Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, kuingia madarakani, Lowassa aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu, kwa maana ya kiongozi wa shughuli za serikali bungeni na mtendaji mkuu wa serikali.

Hapo pia hakuwa na mzaha katika utekelezaji wa majukumu yake na alikemea waziwazi kuhusu uvivu huku akimtaka kila mtu aliyepewa dhamana kufanya kazi. Wakati wa mikutano ya Bunge, mawaziri walikuwa na wakati mgumu walipobanwa na wabunge na wakati mwingine kiti cha akiba cha karibu yake bungeni kilikuwa kikionekana cha moto kutokana na wabunge na mawaziri wa CCM kuitwa mara kwa mara.

Hali hiyo pia ilijitokeza alipotikisa baada ya kujitoa katika Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015 baada ya jina lake kukatwa alipowania kugombea urais na hatimaye kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) hatimaye kuteuliwa kuwa mgombea urais akiwakilisha uliokuwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Umoja huo ulikuwa ukiwakilisha, mbali na CHADEMA, Chama cha Wananchi (CUF), NCCR-Mageuzi na National League for Democracy (NLD).

Lowassa hakuondoka CCM peke yake kwa kuwa alifuatana na wanasiasa wengi mashuhuri wakiwamo aliyewahi kuwa Waziri Mkuu katika serikali ya awamu ya tatu, Frederick Sumaye, na mwanasiasa mkongwe Kingunge Ngombale Mwiru.

Hali iliyoonyesha kuwa uchaguzi wa mwaka 2015 ungekuwa na vuta nikuvute, ni pale msafara wake kutoka ofisi za CUF, Buguruni kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwenda kuchukua fomu na hatimaye kutoka NEC (katikati ya jiji la Dar es Salaam) kwenda makao makuu ya CHADEMA, Kinondoni, alipoandika historia kwa watu kujaa barabarani na msururu wa magari kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Hata katika mikutano yake ya kampeni iliyokuwa ikivuta umati wa watu katika maeneo mengi nchini, ilionyesha dhahiri kwamba Lowassa ni chuma.

**TAARIFA YA KIFO**

Rais Samia Suluhu Hassan, jana alitangaza kifo cha mwanasiasa huyo aliyejipatia umaarufu tangu enzi za ujana wake kuwa alikutwa na umauti wakati akipatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Akiwatangazia Watanzania kwa niaba ya Rais Samia jana akiwa mkoani Arusha, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema Lowassa alifariki jana majira ya saa 8:00 mchana.

"Naomba radhi kwa kuchelewa kidogo kwa kuwa baada ya kufika nililazimika kwenda kufanyia kazi dharura ya kitaifa ndiyo maana nimechelewa kufika hapa. Na kwa sababu hiyo nimetoka kulitangazia taifa letu kwamba siku ya leo (jana) saa 8:00 mchana, tumempoteza kiongozi wetu aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa.

"Lowassa alikuwa akipatiwa matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kabla ya mauti kumfika. Awali alipelekwa Afrika Kusini, lakini alirejeshwa tena kwenye Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, hivyo kwa niaba ya Rais Samia, nasikitika kutangaza kifo cha Lowassa," alisema Dk. Mpango.

Makamu wa Rais alisema Rais Samia ametoa pole kwa familia, ndugu,jamaa, marafiki, Watanzania na taifa kwa ujumla kwa msiba huo.

Kutokana na kifo hicho, Dk. Mpango alisema Rais ametangaza siku tano za maombolezo na bendera zote zitapepea nusu mlingoti kuanzia jana na serikali itaendelea kutoa taarifa zaidi za msiba.

**●Imeandikwa na Allan Isack (ARUSHA) na Mwandishi Wetu (DAR)**

## Mambo aliyoyaamini na kuyasisitiza

**Na Gwamaka Alipipi**

ELIMU, elimu, elimu. Ilikuwa kauli ya Edward Lowassa kuonyesha kuwa elimu ni kipaumbele muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Enzi za uhai wake, Lowassa mara kwa mara alikuwa akisisitiza umuhimu wa serikali kuwekeza katika elimu akiamini kwamba ndiyo mkombozi kwa taifa kuondoka katika umasikini. Alikuwa akisema kwake kipaumbele cha kwanza ni elimu, cha pili elimu na cha tatu elimu.

Pia alikuwa akitoa ushauri kwa serikali kufanya tathmini upya mfumo wa elimu nchini, ili kuona kama bado unafaa au la.

Kutokana na umuhimu wa elimu, Lowassa aliwahi kupendekeza kuundwa kwa tume ya elimu kwa ajili ya kufanya tathmini ya mfumo wa elimu, akisema nchi zote zilizoendelea duniani zimekuwa zikifanya hivyo.

**ALIHIMIZA AJIRA**

Vilevile Lowassa alikuwa akisisitiza umuhimu wa kutengeneza mfumo imara wa kuwawezesha vijana kuajiriwa ama kujiajiri.

Baadhi ya nyakati Lowassa alikuwa akisikika akisema 'bomu la ajira kwa vijana linalipuka muda wowote'

Mara nyingi alikuwa akitaka serikali kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo la ajira akisema ni lazima serikali itengeneze ajira kwa wananchi wake, huku akimtolea mfano aliyekuwa Rais wa Marekani, Barack Obama kwamba alishinda awamu ya pili kwa sababu ya kutengeneza ajira.

**ALIAMINI KATIKA KAZI**

Mbali na kuamini katika umuhimu wa elimu na ajira, Lowassa alikuwa muumini katika ufanyaji kazi, akiamini kwamba ili taifa lolote liweze kupiga hatua katika maendeleo ni lazima wananchi wake wawe wachapakazi.

Lowassa alisikika katika vyombo vya habari mara kwa mara akitoa ushauri kwa Watanzania kujielekeza katika kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo badala ya kukaa vijiweni na kuwajadili watu, akisema jambo hilo haliwezi kuwapa tija yoyote.

**HISTORIA YAKE**

Lowassa alizaliwa Agosti 26, 1953 katika kijiji cha Ngarash, Monduli. Alianza masomo katika Shule ya Msingi Monduli mwaka 1961 hadi 1967, baadaye aliendelea na Shule ya Sekondari Arusha kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kati ya mwaka 1968 hadi 1971. Baada ya hapo, alijiunga na masomo ya kidato cha tano na cha sita katika Shule ya Sekondari Milambo, Tabora mwaka 1972 hadi 1973.

Lowassa alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1974 hadi 1977 na kuhitimu Shahada ya Sanaa katika Elimu. Baadaye, alijiunga na Chuo Kikuu cha Bath, Uingereza akisomea Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Maendeleo mwaka 1983 hadi 1984.

**KAZI**

Baada ya kumaliza elimu ya juu, Lowassa alifanya kazi katika Chama Cha Mapinduzi (CCM) akiwa ofisa wa ngazi ya juu kuanzia wilaya, mkoa na baadaye makao makuu ya chama kuanzia mwaka 1977 hadi 1989.

Aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC) kuanzia mwaka 1989 hadi 1990.

Lowassa alichaguliwa kuwa mbunge wa Taifa mwaka 1990 na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (Haki na Mambo ya Bunge) hadi mwaka 1993 kabla ya kuwa Waziri wa Ardhi na Makazi mwaka 1993 hadi 1995.

Aligombea ubunge katika jimbo la Monduli mwaka 1995 na kushinda. Mwaka 1999, aliteuliwa na Rais Benjamin Mkapa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Kuondoa Umasikini). Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, aligombea tena ubunge Monduli na kushinda kisha Rais Mkapa alimteua kuwa Waziri wa Maji na Mifugo hadi mwaka 2005. Katika uchaguzi wa mwaka 2005, Lowassa aligombea tena ubunge Monduli na kushinda kwa kishindo na katika serikali ya awamu ya nne chini ya Rais Jakaya Kikwete, aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu na Bunge lilimthibitisha kwa kura 312. Uwaziri Mkuu ulikoma mwaka 2008 alipojiuzulu kutokana na kashfa ya Richmond.

Lowassa ameacha mjane aitwaye Regina, watoto watano, wasichana wawili, wavulana watatu ambao ni Fredrick, Pamella, Adda, Robert na Richard.

## LOWASSA 1953-2024



Waziri Mkuu mstaafu, Edward Ngoyai Lowassa akiwa katika moja ya mikutano yake ya kisiasa katika Chama Cha Mapinduzi (CCM), enzi za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

# Samia, Mwinyi wamlilia Lowassa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wamemlilia aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, aliyefariki dunia jana jijini Dar es Salaam.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram, Rais Samia aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Ngoyai Lowassa.

Rais aliandika kuwa Lowassa aliitumikia Tanzania katika nafasi mbalimbali kwa zaidi ya miaka 35, akianzia ushiriki wake katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Chama Cha Mapinduzi (CCM), mbunge, waziri katika wizara mbalimbali na Waziri Mkuu.

Pia aliandika: "Tumempoteza kiongozi mahiri aliyejituma na kujitoa kwa nchi yetu. Natoa pole kwa mjane mama Regina Lowassa, watoto (Mh.Mbunge wa Monduli, Fredrick Lowassa na wadogo zake), ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huu mzito.

"Katika mawasiliano yangu na familia, nimewaeleza kuwa kama taifa tuko pamoja nao katika kipindi hiki kigumu, kamwe wasiache kumtegemea Mwenyezi Mungu na kutafakari neno lake hasa kitabu cha Ayubu 1: 21".

**KAULI YA MWINYI**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Lowassa kilichotokea jana katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete alipokuwa akipata matibabu.

Lowassa alikuwa akisumbuliwa na matatizo ya mapafu na shinikizo la damu hadi alipofariki dunia.

Kutokana na kifo hicho, Rais Dk. Mwinyi alisema anaitakia familia ya marehemu Lowassa, ndugu na marafiki moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

Alimwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. Amin.

Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alirejea maneno hayo ya Rais na baadaye kuandika katika ukurasa wake wa X (zamani Twitter) kuwa: Nimesikitishwa sana kusikia msiba wa Mzee Edward Ngoyai Lowasa, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania.

"Salaam zangu za rambirambi ziwe pamoja na familia yake wakati huu mgumu kwao. Mungu awape nguvu na mshikamano wa dhati. Poleni wana Monduli na Arusha."

Boniface Jacob, Meya wa zamani wa Ubungo, aliandika kuwa jabali la siasa limeondoka na kumwelezea kuwa ni mtu muungwana ambaye ametangulia.

"Rafiki amelala usingizi wa milele. Kiongozi wa watu ametamatika. Mzee Lowassa ilikuwa shule ya siasa na uongozi iliyokuwa inatembea, tuliobahatika kuwa naye karibu tumeachiwa utajiri wa maarifa. Nawapa pole ndugu, jamaa, marafiki pamoja na familia ya Mzee Edward Ngoyai Lowassa."

Mchambuzi wa siasa za Tanzania na Afrika, Hamduni Maliseli, alisema kifo cha Lowassa kimeacha alama kubwa ndani na nje ya nchi kwa kuwa atakumbukwa kwa misimamo yake kwa nyakati tofauti za ungozi wake katika nafasi mbalimbali.

Alisema akiwa Waziri wa Maji Lowassa aliingia katika mvutano mkubwa uliohusisha serikali za Misri na Tanzania kuhusu mkataba wa zamani wa kimataifa uliokuwa unaipa Misri hakimiliki ya Ziwa Victoria kutokana na Ethiopia, Misri na Sudan kutegemea Mto Nile ambao chimbuko lake ni katika ziwa hilo.

"Wakati huo Tanzania ilitaka kuanzisha mradi wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria Kwenda katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Dodoma na Singida lakini ilikuwa vigumu kulingana na matakwa ya mkataba huo wa kimataifa. Lowassa aliweka msimamo na akizitaka nchi hizo pia kuipa Tanzania umiliki wa mafuta kama zitaweza. "Kauli hiyo aliitoa katika Mkutano wa Cairo na kusema ni lazima Tanzania itumie maji hayo kuwanufaisha Watanzania. Lakini pia Lowassa alikuwa muumini wa sera ya elimu ni miongoni mwa watu waliosimamia ujenzi wa madarasa pamoja na madawati akiamini kuwa bila elimu hakuna maendeleo ya nchi," alisema Maliseli.

Pia alitaja misimamo yake iliyodhihirisha na kutoa fundisho juu ya suala la demokrasia nchini ikiwa ni pamoja na kuwajibika akiwa kiongozi wakati huo alipokuwa Waziri Mkuu na kujiuzulu pia kuhama chama tawala na kutafuta maisha katika chama pinzani.

"Alitoa somo kwa chama tawala kuwa vyama vya upinzani si dhambi kila mtu anaweza kuwa kwenye chama chochote kwa mujibu wa haki yake ya kikatiba na hii tuliona alivyofanya vizuri katika uchaguzi huo mkuu," alisema.

**SIMAI NDANI**

Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, Simai Mohamed Said ambaye ni rafiki mkubwa wa Lowassa, alisema amepokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha mwanasiasa huyo huku akieleza kuwa amejuana naye kabla hajawa Waziri Mkuu kwa kuwa amesoma shule moja na mtoto wake, Fredrick.

Alisema kujuana kwao kulisababisha wakawa marafiki wa familia na kila Lowassa alipofika Zanzibar, ikiwamo wakati wa Krismasi na Pasaka, ilikuwa lazima wakutane.

"Tokea hajaanza mchakato wa kutaka kugombea urais mwaka 2015, alikuwa na tabia ya kuja Zanzibar mara kwa mara na familia yake na alikuwa mwanasiasa mzuri anayejichanganya na vijana na unapokaa naye, unajisikia kama uko mtu na rafiki yako," alisema Simai ambaye hivi karibuni alikuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale kabla ya kujiuzulu.

Pia alisema amejifunza mengi kutoka kwake na alipokuwa akipatiwa matibabu Afrika Kusini, alikwenda kumwona na kumwombea dua na atamkumbuka daima miongoni mwa viongozi na wanasiasa ambao walikuwa na ushawishi mkubwa.

**● Imeandikwa na Gwamaka Alipipi, Vitus Audax na Rahma Suleiman**

## CCM, ACT Wazalendo zatuma salamu za pole

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) na ACT- Wazalendo vimetuma salamu za rambirambi kwa familia ya mwanasiasa Edward Lowassa kutokana na kifo chake jana huku vikisema atakumbukwa kwa mambo mengi amekuwa kiongozi mwema kwa nafasi zote alizozishika.

Akiwa mkoani Ruvuma, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, alisema: "Niungane na Mwenyekiti wetu wa chama na Rais Samia Suluhu Hassan, kutoa pole kwa niaba ya chama chetu kwa familia ya mzee wetu Lowassa kwa kuondokewa na mpendwa, kiongozi wetu na mwanachama wetu aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu ambaye amefariki leo (jana)."

Makonda alisema kwa niaba ya CCM wanatoa pole kwa wanachama, wapenzi wa chama, wakereketwa na Watanzania wote kwa ujumla na kwamba Lowassa amekuwa kiongozi mwema kwa nafasi zake zote ametoa mchango kwa taifa.

Makonda alisema Lowassa atakumbukwa kwa mambo mengi kwa umahiri wake wa kujenga hoja kwa nyakati tofauti wamekubaliana na uamuzi wa Mwenyezi Mungu.

Mkurugenzi wa Uenezi na Mawasiliano wa ACT Wazalendo, Salum Bimani, alisema ni msiba mzito kwa taifa na Watanzania kwa sababu alikuwa mtumishi wa muda mrefu kwa nafasi mbalimbali.

Alisema Lowassa alipokwenda upinzani walisimama naye vizuri licha ya uchaguzi kuchafuliwa lakini kazi kubwa ilifanyika ni mtu mtulivu, mwenye busara na mawazo.

"Tunatoa pole kwa familia, Watanzania, watu wa Monduli na kwa Rais Samia na wale wote waliofanya kazi naye. Hata alipokuja katika upinzani alituimarisha licha ya baadae kurejea CCM," alisema.

Pia alisema hata alipoondoka katika upinzani hakuwa na kebehi au kuutukana, hivyo wataendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika siasa na hata taifa.

Aidha, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Vuai Ali Vuai, alisema wamepokea kwa masikitiko makubwa kifo hicho kwa sababu alikuwa kiongozi CCM na kwa muda mrefu alikuwa kiongozi wa kitaifa kwa nafasi ya Waziri Mkuu na ametumikia nchi kwa kipindi kirefu na mchango wake kwa taifa ni mkubwa.

"Sisi wana CCM hatuwezi kusahau mchango wake alioutoa kwa taifa lake kipindi anatumikia nchi. Amefanya kazi kubwa kwa kipindi kirefu. Mchango wake kwa Tanzania ni mkubwa, hauwezi kusahauliwa," alisema.

Alisema alifanya kazi naye kwa karibu hasa kipindi Lowassa akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Wadhamini la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) wakati huo yeye akiwa katibu mkuu wa jumuiya hiyo, hivyo alikuwa karibu naye.

**●Imeandikwa na Beatrice Shayo na Rahma Suleiman**

HABARI KITAIFA

DK. ZEPHANIA KAMEETA

# Askofu, mwanasiasa aliyepita milima na mabonde

## -Ni mwenye ualbino, aliwahi kuwekwa kizuizini na kufungwa

**Na Mwandishi Wetu**

NI mwenye ualbino, kasisi na askofu, mfungwa wa kisiasa, mwanasiasa, mpigania uhuru na haki za binadamu. Hivyo ndivyo anavyoweza kuelezewa kutokana na historia ya maisha yake.

Huyo si mwingine bali ni Askofu Dk. Zephania Kameeta (79), raia wa Namibia ambaye kutokana na historia yake, amejijengea umaarufu tangu akiwa kijana. Ni kiongozi wa kiroho, kisiasa na kijamii aliyejipambanua kujali zaidi jamii kuliko maisha yake na ya familia yake kwa ujumla.

Wakati wa harakati za ukombozi wa Namibia, Dk. Kameeta, ambaye kwa sasa ni Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri la Jamhuri ya Namibia (ELCRN), alikuwa mstari wa mbele. Pamoja na hali yake ya ualbino, hakujali kuhatarisha maisha yake. Hata katika hotuba zake kwenye makongamano mbalimbali, alikuwa mstari wa mbele kuhamasisha Namibia na Afrika Kusini kuwa huru dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi.

Harakati zake hizo zilisababisha kukamatwa, kuwekwa kizuizini na hata kufungwa. Pia kutokana na kupinga waziwazi ubaguzi wa rangi na aina mbalimbali za ukandamizaji, mara kadhaa aliwahi kunyang'anywa hati yake ya kusafiria na serikali ya Afrika Kusini, wakati wa utawala wa makaburu.

Huenda maisha ya Askofu Kameeta yanaakisi hali halisi ya kihistoria kutokana na kuzaliwa mwishoni mwa Vita vya Kwanza vya Dunia (1945). Pia kukua na kushiriki kwake katika harakati za ukombozi wa Namibia, ni vita vingine vilivyofanya awe kama alivyo, ambavyo alijiunga navyo baada tu ya kumaliza masomo yake ya theolojia na baadaye kuwa mchungaji na hatimaye Askofu.

Sifa nyingine iliyomfanya apate umaarufu na kukubalika kwa jamii ndani na nje ya Namibia ni hali yake ya ualbino ambayo alitumia kuwasaidia watu wa kundi hilo kujulikana na kukubalika ndani ya jamii kama walivyo binadamu wengine.

Wakati mauaji ya watu wa jamii hiyo yakishika kasi katika maeneo mbalimbali Afrika, Tanzania ikiwamo, alikuwa mstari wa mbele kutumia majukwaa aliyokuwa nayo kukemea vitendo hivyo na kufanya kampeni ya kutambuliwa kwa watu hao.

### UCHUNGAJI NA SIASA

Baada ya Namibia kupata uhuru mwaka 1990, Kameeta alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge wa kwanza.

Katika miaka 10 akiwa kwenye nafasi ya Naibu Spika, alipata umaarufu mkubwa katika jamii kutokana na kuonekana mara kwa mara kwenye vituo vya televisheni hususan kwenye mijadala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Hapo ndipo alipoonekana kuwa mtu mwenye ualbino lakini mwenye uelewa mpana wa mambo mbalimbali ya kisiasa na kijamii.



Mwaka 2000, baada ya kumaliza muda wake, alitoweka ghafla na hakuonekana tena kwenye mikusanyiko mbalimbali wala kujulikana aliko. Ni watu wa karibu yake pekee waliojua aliko kabla ya kubainika baadaye kuwa alikuwa kusini mwa Namibia, mji mdogo wa Maltahohe, wenye umaskini uliotopea, uliopoteza mamia ya watu kutokana na UKIMWI, akifanya kazi kama mchungaji wa kujitolea. Akiwa anajitolea, pia alikuwa mratibu wa shirika la kimataifa la masuala ya uenezaji injili la United Evangelical Mission (UEM).

Hakujali historia yake wala nafasi yake zaidi ya ubinadamu. Pamoja na kuwa katika nafasi kubwa kisiasa awali, aliamua kurudi kwa wananchi, akifanya kazi bila mshahara tena katika usharika maskini katika nchi yake.

"Akiwa huko, mara nyingi alikuwa akizitembelea familia zisizo na kipato, wagonjwa na yatima kwenye vibanda na mitaani, huku akisikiliza vilio vyao kuhusu mateso, maumivu na magonjwa, njaa na umaskini," ilieleza taarifa moja kuhusu maisha yake.

### KISHINDO KIKUBWA

Kama maandiko matakatifu yasemavyo ajishushaye atakwezwa, Januari 20, mwaka 2002, Dk. Kameeta aliibuka kwa kishindo na kuonekana tena katika jamii akiwekwa wakfu kuwa Askofu.

"Niko juu tena," alisema Dk. Kameeta baada ya kubarikiwa na kuwekwa wakfu kuwa Askofu huku akionyesha kuwa huko si kupanda na kuwa mtu maarufu bali ni kama adhabu kwake. Hakuiona nafasi hiyo kama sehemu ya kunufaika wala kujipatia umaarufu.

Alitamka wazi kwamba: "Nitapenda zaidi kuwa karibu na watu (wa hali ya chini) kuliko awali. Kiongozi anayejitenga na kutokuwa na mawasiliano na watu wa chini, huyo ni mtu aliyeshindwa."

Hali hiyo ilisadifu na kauli yake. Kumtafuta Askofu Kameeta katika ofisi yake katikati ya Windhoek ilikuwa rahisi hata milango katika jengo la utawala la kanisa lililoliongoza ilikuwa wazi na ofisi yake ilikuwa wazi zaidi- hakukuwa na kizuizi cha kumwona bila kujali nafasi wala hali ya aliyetaka kumwendea, wakati wote akiwa katika mavazi ya kiaskofu na tabasamu tele.

### RAIS AMWAGIA SIFA

Wakati akistaafu utumishi wa kanisa kama Askofu, Dk. Kameeta alimwagiwa sifa kemkem na Rais wa nchi hiyo, Hage Geingob, akimwelezea kuwa ni mtu mwenye historia ya kipekee na mmoja watu mashuhuri katika nchi hiyo. Dk. Geingob aliyefariki dunia wiki iliyopita, alimteua Dk. Kameeta katika baraza lake la kwanza kuwa Waziri wa Kuondoa Umaskini na Ustawi wa Jamii.

Katika hafla iliyoandaliwa kumpongeza kwa utumishi wake mwema, kiongozi huyo alimwelezea Askofu Dk. Kameeta kuwa hakutoa mchango chanya kwa watu wa Namibia pekee bali hata katika safari ya maisha yake mpaka kuwa Rais wa nchi. Rais Geingob katika hafla hiyo aliwakilishwa na aliyekuwa makamu wake, Dk. Nangolo Mbumba, ambaye kwa sasa ni Rais wa Nambia baada ya kifo cha kiongozi huyo.

"Askofu Dk. Kameeta ni kiongozi na mtumishi wa kweli na 'Shujaa wa Namibia, asiye na ukabila, mzalendo wa kweli, mpenda nchi yake, mtu anayechukia rushwa na uovu na mtu wa kujishusha aliyejitolea maisha yake kwa ajili ya watu maskini na waliosetwa," alisema.

Dk. Geingob alisema kwa mara ya kwanza alikutana na Askofu Kameeta mwaka 1970 katika Taasisi ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Namibia (UNIN), Lusaka nchini Zambia ambako yeye (Geingob) alikuwa mkurugenzi akiwa uhamishoni.

Walipokutana, alisema Kameeta alionyesha ni mwanamapinduzi wa kweli alipowaambia wanafunzi wa UNIN kuwa: "Uongozi si kuvaa kola shingoni, unakuja na uwajibikaji na majukumu."

Kwa mujibu wa Geingob, ilikaa katika kumbukumbu zake na kwa kiasi kikubwa ilimpatia uelewa kuwa uongozi si kujionyesha au kujivuna bali ni wajibu unaotaka mtu kuwa na utu, uwazi na uwajibikaji.

Kutokana na msimamo usioyumba wa Dk. Kameeta, Geingob alibainisha kuwa wakati akisubiri matokeo ya uchaguzi wa SWAPO katika kinyang'anyiro cha urais wa Namibia, akiwa mmoja wa wanaowania nafasi hiyo, baadhi ya watu ndani ya chama hawakutaka kuwa karibu naye.

Hata hivyo, alisema Bishop Kameeta baada ya matokeo, alipanda jukwaani na kuueleza umma kwamba: "Mimi na mke wangu tuko hapa kumzungumzia Hage, Hage ambaye tunamjua si Hege 'mliyemfanya (kumchagua). Kauli hiyo ilinifanya niwe mtu wa aina yake katika majukumu ya uongozi.

"Kupitia kauli hiyo, nilipata nguvu na ujasiri na kwa kutambua tabia ya Askofu Kameeta kutokua na ubinafsi, nilipochaguliwa kuwa Rais, niliamua kuunda wizara ya kuondoa umaskini na ustawi wa jamii ambayo ilikuwa na jukumu kubwa kwa taifa kutokana na hali halisi ya Namibia.

Kwa kushika wadhifa huo, alikiri kwamba Askofu Kameeta alifanya mambo makubwa yaliyoleta tofauti katika maisha ya maelfu ya wananchi wa Namibia kupitia programu na mipango kama kuanzisha benki ya chakula.

"Hata nilipoamua kuifuta wizara hiyo na kuanzisha Wizara ya Jinsia, Kuondoa Umaskini na Ustawi wa Jamii, Askofu Kameeta hakulalamika bali alikubali hali iliyoonyesha kuwa si mtu mwenye ubinafsi," alibainisha.

### HISTORIA YAKE

Askofu Dk. Kameeta, ambaye alizaliwa Agosti 7, 1945 katika Otjimbingwe, mkoa wa Erongo, ana historia ndefu katika uongozi wa dini na siasa. Baada ya kustaafu katika nafasi ya uaskofu (kwa maana ya uongozi), aliteuliwa katika serikali ya awamu ya tatu ya Namibia chini ya Geingob kuwa Waziri wa Kuondoa Umaskini na Ustawi wa Jamii.

Kameeta alisomea masomo ya theologia katika Chuo cha Theolojia cha Paulinum, Otjimbingwe nchini Namibia mwaka 1968 hadi 1971. Mwaka uliofuata, alibarikiwa kuwa Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Namibia. Mwaka 1973 alikuwa mhadhiri katika chuo hicho na baadaye kuwa mkuu wake kuanzia mwaka 1976 hadi 1978.

Mwaka 1978, alihamishwa kwenda kuwa Mchungaji Kiongozi Luderitz hadi mwaka 1981 kabla ya mwaka 1982 kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa kanisa hilo na baadaye Askofu Msaidizi mwaka 1985.

Historia yake inaonyesha kuwa mwaka 2002 alichaguliwa kuwa Askofu wa kanisa la Kiinjili la Kilutheri katika Jamhuri ya Namibia (ELCRN), nafasi aliyodumu hadi mwaka 2013 kutokana na umri uliowekwa kikatiba na kanisa hilo.

Aidha, mwaka 2003 hadi 2010, alikuwa Makamu wa Rais wa Fungamano la Makanisa Kilutheri Duniani (LWF) Kanda ya Afrika.

Katika nyadhifa za kisiasa, mwaka 1975, Kameeta alianzisha kundi lililojulikana kama Namibia National Convention, kwa ajili ya kuhamasisha watu weusi kujitambua katikati ya utawala wa kikoloni na ubaguzi wa rangi.

Kundi hilo liliamsha harakati za Waafrika kujikomboa na alikamatwa na mamlaka za Afrika Kusini kwa kupinga Mkutano wa katiba uliokuwa akifanyika Turnhalle.

Pia aliwekwa kizuizini na kufungwa na serikali ya Afrika Kusini ya wakati huo.

Pia aliwahi kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Ukombozi cha Namibia cha SWAPO (sasa chama tawala tangu nchi iwe huru) kuanzia mwaka 1977 hadi 2002. Baada ya Namibia kuwa huru mwaka 1990, alichaguliwa kuwa Mbunge kupitia SWAPO na kuchaguliwa kuwa naibu spika wa bunge na mjumbe wa kamati kuu ya SWAPO hadi mwaka 2002 alichaguliwa na kuwekwa wakfu kuwa Askofu.

Mbali na nyadhifa hizo za kisiasa, Dk. Kameeta Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Hifadhi ya Jamii ya Namibia.

**●Askofu Dk. Kameeta ni mtu wa uwazi katika kila nafasi aliyoishika. Si mtu wa hofu bali mwenye msimamo. Fuatilia sehemu ya pili Jumapili ijayo.**

HABARI KITAIFA

# Pugu yajizatiti kuongeza ufaulu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Shule ya Sekondari ya wavulana ya Pugu, Juma Orenda, amesema katika kuhakikisha wanalinda heshma ya ukongwe wa shule hiyo wameweka mikakati ya kuwa na ufaulu wa daraja la kwanza na la pili.

Amesema wamelazimika kuweka mkakati baada ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne uliopita wanafunzi 15 kupata daraja la tatu, huku shule hiyo ikiwa na historia ya kutoa viongozi wakubwa wa nchi.

Orenda alisema ni kweli shule yake imekuwa ikifanya vizuri na kupata matokeo mazuri.

"Kutokana na hali hiyo basi, mimi pamoja na menejimenti yangu tumejipanga vizuri katika kuhakikisha matokeo yajayo tunapata daraja la kwanza na la pili, huku kufuta matokeo ya daraja la tatu na la nne kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita," alisema.

Alisema kwa wanafunzi waliopata ufaulu mbaya uongozi wa shule itawamudu na kuhakikisha wanarudi kwenye mstari wa kufanya vizuri zaidi.

"Malengo yote haya yatafikiwa kwa kwa nguzo mbili ambazo mojawapo ni nidhamu kwa wanafunzi, walimu pamoja na kudhibiti nidhamu kwa wafanyakazi wasiokuwa waadilifu, lakini pia kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma mzuri kwa watoto wa kitanzania ambao kimsingi ndio wateja wao," alisema.

Kuhusu nidhamu, alisema kuwa kuna kikosi cha dhabiti cha ushauri nasaa na kuna ofisi maalum inayofanya kazi vizuri kwa makuzi, kwamba kuna ushirikishaji mzuri wa wazazi na kila darasa kuna jukwaa lake.

Alisema miundombinu ya walimu imeboreshwa kwa kuweka mizuri katika sekta ya elimu, huku fedha za kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum katika shule yake zikiendelea kutolewa.

Orenda alisema wamekuwa wakitoa jaribio la mitihani kwa wanafunzi kwa wanafunzi kufanya mitihani ya masomo mawili kila wiki, lengo ni kuwa na mzunguko wa mitihani nane kila mwezi bila kuathiri ratiba ya shule.

Pia alisema kuna mitihani maalum ya Mkuu wa Shule kwa vidato vya mitihani ambao unatungwa na wataalam kutoka nje ya shule kwa ajili ya kupima uwezo wa watoto.

Alisema tayari ameunda timu maalum ya taaluma shuleni hapo kwa ajili ya kufanya ziara katika shule zinazofanya vizuri, ili kujifunza.

# Bunge laishukia halmashauri mkopo bil. 1.5/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

KAMATI ya Kudumu ya Bunge,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida kuweka mkakati wa kurejesha haraka Sh. bilioni 1.5 ilizokopeshwa na Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha mashamba ya korosho.

Kamati pia imeiagiza halmashauri hiyo kutoa taarifa inayojitosheleza ambayo itaeleza kwa kina kuhusu mradi huo ili kujua changamoto na kama kuna matatizo ieleze ni nani alisababisha hilo na hatua gani zimechukuliwa.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Justin Kamonga, akitoa maazimio ya kamati jana baada ya wabunge kutembelea mashamba ya mradi huo na kutoridhishwa na hali ilivyo, alisema taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni,Jimson Mhagama haijitoshelezi.

"Kufiatia maelezo yaliyopi kwenye taarifa mliyotusomea kamati inashindwa kushauri kuhusu mradi huu kwa hiyo tunaitaka halmashauri iwasilishe taarifa nyingine kwa kamati kabla ya vikao vya bajeti havijaanza Machi, 2024. Fedha hizi ni mkopo tunahitaji mkakati wa halmashauri jinsi ya kuzirejesha," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Tabora, Hawa Mwaifunga, alisema kwa jinsi ilivyo halmashauri hiyo haiku makini katika mradi huo ndiyo maana katika Sh. bilioni 1.5 ilizokopeshwa tangu mwaka 2021, imerejesha Sh. milioni 365.9 tu. "Mkurugenzi hizi fedha tunazihitaji kama tulivyokubaliana. Fedha hizi ni za wananchi zinahitajika na sehemu nyingine msifikiri ni Manyoni tu ambao mnazihitaji. Haiwezekani tangu 2021 ni karibu miaka minne sasa hamwonyeshi Dalglish kuzirejesha. Angalieni tusije tukakosesha bajeti yenu," alisema.

Naye Mbunge wa Buchosha, Erick Shigongo, alishauri iundwe kamati maalum kufuatilia madeni ya Sh. milioni 332 ambazo wanadaiwa wananchi waliouziwa mashamba mapya lakini hawajalipia na pia halmashauri itangaze mradi huu ili watu wengi wajitokeze kununua mashamba. Mbunge wa Temeke, Dorothy Kilave, alisema inatia shaka kama fedha zilizokopeshwa kwa halmashauri hiyo zitarejeshwa kwasababu kati ya ekari 969.44 zilizotejeshwa kwa kwa wakulima waliokuwa wanaidai halmashauri ekari 479 zimefanywa kuwa barabara.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga, Mwantumu Zodo, alisema inashangaza kuona kasi ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni katika urejeshaji wa fedha walizokopesha ni ndogo wakati zipo halmashauri nyingine ambazo zilikopesha pamoja na Manyoni zilishamaliza kulipa mkopo huo.

"Suala la kusafisha mashamba ni kazi yao sisi tunachotaka ni pesa hii kasumba ya halmashauri kurejesha kidogokidogo mkopo sio sawa,halmashauri ipo hali mbaya katika kurejesha fedha hizo za mkopo,"alisema.

Mbunge wa Mbulu Mjini, Zacharia Massaay, alisema taarifa ya halmashauri haijitosheleszi kwani haijaeleza kampuni iliyopewa zabuni ya kusafisha mashamba hayo ilianza lini kazi hiyo na ilitakiwa kumaliza lini.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alisema kimsingi mradi huu makosa yalifanyika tangu mwanzo kwani awali gharama za kusafisha shamba ziliwekwa kuwa ni Sh.20,000 hadi 60,000 lakini baadaye ikaja kubainika kiasi hicho ni kidogo kikaongezwa hadi kufikia Sh.273,000 kwa kila shamba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jimson Mhagama, alisema hadi kufikia Februari 7, mwaka huu, ekari 1,396 zenye thamani ya Sh. milioni 698 zimeuzwa na Sh, milioni 365.9 zimeshakusanywa na kiasi ambacho bado ni Sh. milioni 332.



Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Florian Mtey akizungumza na wakufunzi wa Shule ya Polisi Moshi (PTS), mkoani Kilimanjaro jana, wakati akifunga mafunzo ya kuelimisha askari polisi kuhusu nafasi zao za kiutendaji katika kulinda mali za watalii na raia ili kukuza shughuli za utalii. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Huduma za afya Mtanzania alipo mwaka 2030

**Na Allan Isack,** LONGIDO

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema ifikapo mwaka 2030, kila mwananchi atafikiwa na huduma za afya mahali anapoishi, lengo likiwa kurahisisha upatikanaji na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana wakati akizindua Kituo cha Afya Ketumbeine, Longido mkoani Arusha pamoja na kuwasha umeme kwenye kituo hicho kama ishara ya kuzindua mradi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Pia aliweka jiwe la msingi katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido ya Samia Suluhu Hassan.

"Serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan inaendelea kugusa maisha ya kila Mtanzania katika sekta ya afya. Imejipanga kuimarisha huduma za afya na ifakapo mwaka 2030, kila mwananchi atakuwa amefikiwa na huduma alipo," alisema.

Makamu wa Rais aliipongeza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), uongozi wa mkoa wa Arusha na mkandarasi kwa aliyejenga kituo hicho kwa ubora na kiwango kulingana na thamani ya fedha.

"Nawapongeza TAMISEMI, mkandarasi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ujenzi wa jengo hili zuri linalogharimu Sh. bilioni 1.32 ikiwa ni mpango wa serikali kufikia mwaka 20230 kila mwananchi atakuwa amefikiwa na huduma za afya alipo," alisema.

Katika hatua nyingine, aliiagiza TAMISEMI kuongeza watumishi, vifaa na vifaa tiba pamoja na kupeleka gari la kubeba wagonjwa katika Kituo cha Afya Ketumbeine.

Pia alisema kwa sasa upatikanaji wa dawa katika kituo hicho umefikia asilimia 93.6 huku akiagiza TAMISEMI kuendelea kuongeza dawa na vifaa tiba.

Dk. Mpango alisema baada ya serikali kupitisha Sheria ya Bima ya Afya, kila mwananchi atapata huduma za afya hata asipokuwa na fedha mfukoni, hivyo akasisitiza kila mwananchi kujiunga na bima.

Pia aliagiza TAMISEMI kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Longido, Stephen Ulaya, kujenga chumba cha kuhifadhia maiti kwenye kituo hicho.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema serikali kwa nchi nzima katika sekta ya afya imetoa Sh. trilioni 6.7 kuelekea miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia na mkoa wa Arusha kwenye sekta hiyo, ulipatiwa Sh. bilioni 46.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, anayeshughulikia afya, Dk. Wilson Mahera, alisema mpango wao ni kusogeza huduma za afya mpaka vijijini.

Alisema TAMISEMI imetoa Sh. bilioni 361 kwa ajili ya kujenga zaidi ya majengo 1,000 yakiwamo ya zahanati na vituo vya afya nchini na kwamba tangu mwaka 2020 hadi 2023, imetumia Sh. bilioni 202 kununua dawa na vifaa.

Naye Mbunge wa Longido,ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, Dk.Stephen Kiruswa,alisema kwa wastani kila kata 18 zilizoko wilayani himo imepokea zaidi ya Shilingi tatu .

Alisema kituo kujengwa kwa kituo hicho,kitakwenda kuwa mkombozi kwa wananchi wa eneo hilo,kwa kuwa walikuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita 70 kupata huduma kwa tarafa za jirani.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Said, alisema kupitia kwa wakala huo, serikali imeweka Sh. 73,989,383,423.14 kwa mkoa wa Arusha kwa miradi mitano ya umeme ambayo inayoendelea kutekelezwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti wizi dawa, vifaa tiba

**SERIKALI** imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha huduma za afya zinaimarishwa na kuboreshwa kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, serikali kuanzia awamu ya nne, ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambao unabainisha kuwa kila kijiji kinakuwa na zahanati na kituo cha afya katika ngazi ya kata.

Aidha, katika ngazi ya wilaya, mpango unabainisha kuwapo kwa hospitali ya wilaya ambayo ni ngazi ya rufani ya vituo vya afya na katika mkoa kunakuwa na hospitali ya rufani ya mkoa pamoja na kuwa na hospitali za rufani za kanda na ile ya taifa ya Muhimbili.

Kwa hakika hilo serikali imelifanikisha kwa hali ya juu kwa kuwa hivi sasa mbali na kuwa na hospitali za wilaya, mpango huo sasa umeongezwa wigo wa kuwa na hospitali kila halmashauri. Sambamba na hilo, kuanzia vituo vya afya kuna huduma mbalimbali ambazo zimerahisisha huduma za afya kama vile upasuaji na vipimo mbalimbali ambavyo awali vilikuwa vinapatikana kuanzia ngazi ya wilaya.

Seriakli pia imekuwa ikipeleka dawa na vifaa tiba katika vituo hivyo vya huduma na kuwezesha upatikanaji wa dawa kuwa mzuri. Hali hiyo ni tofauti na ilivyokuwa awali ambapo mgonjwa alikuwa akiandikiwa dawa, anaambiwa hazipo, hivyo aende kununua kwenye maduka binafsi.

Hata hivyo, katika miaka ya karibuni kumekuwa na wimbi la wizi wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya hali ambayo inarudisha nyuma au kuhujumu mipango ya serikali katika azma ya utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Wimbi hilo la wizi wa dawa na vifaa tiba limekuwa sawa na donda ndugu kwa sababu limeenea kila mahali. Kila uchao taarifa za kuibwa kwa dawa na vifaa tiba katika maeneo mbalimbali zimekuwa zikitolewa huku wahusika wakubwa wakiwa watumishi waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali hizo, wakiwamo wafawidhi.

Wiki hii mathalan, mkoani Njombe, Jeshi la Polisi lilitangaza kuwashikilia watu wanne, wakiwamo watumishi wawili na mlinzi kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya ujenzi katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Makambako. Tukio hilo lilidaiwa kutokea Januari 31, mwaka huu, na wanaodaiwa kufanya hivyo ni daktari ambaye alikabidhiwa funguo za stoo na mtunza stoo aliyepewa kazi ya kutunza vifaa hivyo.

Licha ya kuwapo kwa tukio hilo, Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, aliwahi kunukuliwa akisema amegundua wizi wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya, umetapakaa nchini kwa watumishi wa umma kuuziana vifaa hivyo kila vinapoletwa na serikali. Mtaka alisema hayo baada ya kufanya ziara kwenye vituo vya afya mkoani humo na kukuta hakuna vifaa licha ya serikali kupitia wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupeleka vifaa vyenye thamani ya mabilioni ya shilingi.


Katika kuonyesha kuwa tatizo hilo ni kubwa, mwaka jana mganga mfawidhi katika zahanati moja mkoani Songwe, alidaiwa kukamatwa na dawa mbalilmbali za binadamu alizokuwa amezificha kwenye mfuko wa sandarusi akiwa katika mchakato wa kwenda kuziuza katika mji wa Mlowo.

Pia katika Halmashauri ya Buchosa mkoani Mwanza, iliripotiwa mashine ya Ultra Sound yenye thamani ya Sh. milioni 80 kuibwa lakini baada ya kuanzishwa msako, ilirejeshwa. Bunda mkoani Mara, nako ilitolewa taarifa ya kuibwa vifaa tiba vya zaidi ya milioni 500 na wafanyakazi wa hospitali ya wilaya.

Matukio hayo, yanatia doa nia njema ya serikali katika kuendeleza sekta ya afya ambayo ni kiungo muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na maisha ya binadamu kwa ujumla. Ni vyema hatua kali zikachukuliwa kukomesha vitendo hivyo, ikiwamo wanaobainika kufikishwa katika vyombo vya sheria na kupewa adhabu kali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ufugaji samaki kwa vizimba usaidie kuondoa uvuvi haramu

Na Sabato Kasika

**MTINDO** wa baadhi ya wavuvi kutumia sumu, baruti au nyavu zilizopigwa marufuku, ni miongoni mwa sababu ambazo hutajwa kuchangia upungufu wa samaki katika Ziwa Victoria.

Bila wavuvi kujua au kwa kujua, mtindo huo unaweza kuyumbisha uchumi wao kwani uvuvi haramu unachangia kuwapo kwa uhaba wa samaki unaosababishwa na wao wenyewe.

Ikumbukwe kwamba kuvua samaki kwa kutumia sumu au baruti, ni sawa na kuua mazalia ya samaki na pia kuvua kwa kutumia nyavu ndogo zilizopigwa marufuku ni sawa na kuua samaki wadogo.

Nyavu za matundu madogo huwa zinazoa samaki wakubwa na wadogo, kitendo ambacho kinasababisha samaki waendelee kupungua ndani ya ziwa, hivyo ni vyema kupitia ufugaji wa vizimba wavuvi wabadilike.

Kwa ni ni ninashauri hiivyo? Ninashauri wabadilike,kwa sababu serikali imekuja na njia mbadala, ambayo itasaidia kuvua pia kulinda mazalia samaki, ili waendelee kuwapo ndani ya ziwa hilo.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alizindua ugawaji wa vizimba 222 vya ufugaji wa samaki na boti 55 za kisasa kwa vikundi 1213 vya wavuvi wa mikoa ya kianda ya Ziwa Victoria.

Ninaamini hatua zinazochukuliwa na serikali katika sekta ya uvuvi ikiwamo kufuga wa samaki kwa njia ya vizimba, inaweza kumaliza uvuvi haramu ambao miaka ya nyuma ulishamiri kanda ya ziwa.

Kama nilivyoanza kueleza, baadhi ya wavuvi walikuwa wanatumia sumu kuvua samaki na kuhatarisha afya za wateja, lakini pia uvuvi wa baruti na wa nyavu zisizopigwa marufuku vyote ni hatari.

Rais aliweka wazi katika hotuba yake na kutaja baadhi ya mambo yanayofanywa na serikali kuinua uchumi kupitia sekta ya uvuvi na kuwa na mchango kwa pato la taifa kutoka asilimia 1.8 hadi 10 ifikapo 2030.

Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kufanywa na serikali na yanayoendelea kutekelezwa ili sekta hiyo iwe na mchango mkubwa kwa taifa ni kuimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Uvuvi.

Aidha, inaelezwa kuwa serikali inaendelea na mpango wa kuweka miundombinu ya wawekezaji kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi ili kuisaidia sekta hiyo kuongeza uzalishaji na mauzo na kuinua uchumi wa taifa na wananchi wanaofanya kazi katika sekta hiyo.

Ni imani kwamba wavuvi hawana budi kuunga mkono juhudi hizo, kutokana na kwamba baadhi ya wavuvi walikuwa wanatumia sumu kuvua samaki na kuhatarisha afya za wateja, lakini pia uvuvi wa baruti na wa nyavu zisizopigwa marufuku na kusababisha msuguano kati yao na serikali.

Kwa kuwa serikali imeahidi kuendelea kutoa zana za kisasa za uvuvi na ufugaji kwa makundi mbalimbali, wakiwamo vijana na wanawake, ninaamini sasa hakutakuwa na njia ya mkato katika uvuvi.

Uvuvi kwa njia ya mkato ndio ambao ulichangia kuwapo kwa wavuvi haramu waliokuwa wanahatarisha afya za wateja wao kwa kuua samaki kwa njia ya simu na kwenda kuwauza.

Wale ambao watakuwa bado wana mawazo ya kuendeleza uvuvi haramu, ni vyema watambue kuwa serikali imeshaahidi kuendelea kuongeza zana hizo kulingana na matokeo yatakayopatikana kutoka kwa wanufaika. Ninaamini manufaa yatakuwapo, kwani si rahisi kuanzisha mradi ambao haujafanyiwa utafiti.

Hadi mradi kuanzishwa, hatua mbalimbali zitakuwa zimechukuliwa ukiwamo utafiti kuhusu vizimba hivyo.

Kwa kuwa wizara husika ina mpango wa kuweka chombo/wakala atakayesimamia na kuangalia maendeleo ya sekta ya uvuvi na kuwaondolea adha wavuvi, kuna uwezekano wa kufanikiwa.

Hapa ina maana kwamba wenye vizimba na wafanyabiashara hawatalazimika kwenda wizarani kwa ajili ya kutatuliwa kero ambazo zinawakabili, badala yake watamalizana na chombo au wakala.

**FIKRA MBADALA**

# Alichokifanya Simai ni ushujaa, anastahili pongezi



Pascal Mayalla

MOJA ya mambo yaliyotawala katika media ya siasa hivi karibuni ni kujiuzulu kwa Waziri wa Utalii na Mambo ya kale katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Simai Mohamed Said. Hatua ya Simai ambaye ni Mwakilishi wa Tunguu katika Baraza la Wawakilishi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ilipokewa kwa hisia tofauti na wanasiasa na wanaharakati.

Wako waliopongeza kuwa ni uamuzi wa busara baada ya kuona mambo hayaendi vizuri na wengine kumwona kama si mzalendo hasa pale alipotaja sababu kuwa ni mazingira yasiyo rafiki katika kutekeleza wajibu wake.

Pia kuna maswali kwa nini autangazie umma kupitia vyombo vya Habari badala ya kuanza kwa kumpatia barua yule aliyemteua? Swali lingine ni kwa nini amjibu Rais Hussein Ali Mwinyi baada ya kusema alipaswa kutangulia kutoa taarifa kwa Rais? Hilo linaonekana kuwakera viongozi wa chama chake, hivyo kumwita na kumweka kitimoto.

Pamoja na yote hayo, kupitia safu hii, ni wazi kwamba kitendo hicho ni cha ushujaa mkubwa, hivyo anastahili pongezi na kupigiwa mfano badala ya kusakamwa, kusimangwa na kukaliwa vikao.

Kitendo cha Simai kujiuzulu wadhifa wake wa uwaziri bila kuwapo kwa kashfa yoyote, wala shinikizo lolote, ni cha ushujaa wa hali ya juu na kinapaswa kuwa mfano kwa wanasiasa wote wa Tanzania.

Jina la Simai, linaingia moja kwa moja katika historia ya mashujaa wa taifa kwa kuwa mwanasiasa wa pili kujiuzulu wadhifa wake wa kisiasa bila kutokea kashfa yoyote au shinikizo la nje au la ndani. Shujaa wa kwanza kujiuzulu kwa mtindo huu ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1962

Kwa vile si wengi walikuwapo enzi hizo tulipopata uhuru Desemba 9, 1961, japo sote tunajua shujaa wa uhuru wa Tanzania (enzi hizo Tanganyika) ni Mwalimu Nyerere, si wengi wanafahamu kuwa tulipopata uhuru, hatukuwa Jamuhuri, hivyo Nyerere aliyeuleta uhuru wa Tanganyika aliupokea akiwa Waziri Mkuu, hivyo Tanzania ilipopata uhuru wake nchi ilikuwa ikiongozwa na Waziri Mkuu, na Mwalimu Nyerere ndiye alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanyanyika. Mwalimu Nyerere alidumu kwenye wadhifa huo wa Waziri Mkuu wa Tanganyika kwa kipindi cha siku 40 tu. Januari 20, mwaka 1962, Mwalimu Nyerere, bila shinikizo kutoka popote na kwa yeyote, aliamua kujiuzulu wadhifa wa Waziri Mkuu na Rashidi Mfaume Kawawa akateuliwa kushika wadhifa huo. Kitendo cha Mwalimu Nyerere kuiuzulu wadhifa wa Waziri Mkuu, bila shinikizo lolote, ni cha kishujaa sana.

Kwa wanasiasa hiyo ni uamuzi mgumu na ni moja ya sifa muhimu kuwa nayo. Alichofanya Simai ni sawa na uamuzi wa Nyerere.

Katika serikali zinaendeshwa kwa kanuni ya uwajibikaji wa pamoja, ukijiona unatofautiana na wenzako, unapaswa ama kunyamaza ua kupisha kwa kujiuzulu na kukaa pembeni.

Wakati serikali ya awamu ya pili chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi, maarufu kama Mzee Rukhsa, Augustino Mrema, akiwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, alitofautiana na kanuni ya uwajibikaji wa pamoja kwa kulipuka Bungeni kuwa hakubaliani na jambo fulani lililopitishwa ndani ya kikao cha Baraza la Mawaziri. Lyatonga alipaswa kujiuzulu na matokeo yake alifukuzwa.

Simia hakujiuzulu kwa shikizo lolote, watu wenye 'boldness' ya aina hii wanahitajika kwa nchi hii kuitoa ilipo na kuifikisha kule inapaswa kuwa. Wako viongozi wengi waliwahi kujiuzulu, kwa kuandika barua za kujiuzulu, ama kwa shinikizo baada ya kutokea kashfa kwenye wizara zao, kama ile ya mauaji ya vikongwe iliyosababisha kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi , Ali Hassan Mwinyi na Waziri wa Usalama, Peter Siyovelwa.

Pia kuliwahi kutokea kashfa ya sukari, ikasababisha Waziri wa Viwanda Biashara Iddi Simba akajiuzulu. Kashfa ya Richmond pia ilisababisha Waziri Mkuu, Edward Lowassa na mawaziri wa Nishati, Nazir Karamagu na wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki (akliwahi kuwa Waziri wa Nishati), Dk. Ibrahim Msababa walijiuzulu. Mifano hiyo ni kwa uchache.

Aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Yustino Ndugai alipotofautiana na serikali kuhusu mikopo hata akafikia hatua ya kusema kuna siku nchi itapigwa mnada. Kwa kauli hiyo alipaswa awe 'bold' apishe kuliko kuja kujiuzulu kwa aibu. Tulimshauri awe 'bold', aachie ngazi aonekane shujaa, lakini alikomaa akaja kuandika barua ya kujiuzulu kwa shinikizo.

Niliwahi kuandika Makala kuhusu kokosekana wabunge wenye 'boldness' ya aina hii ndani ya bunge letu, hivyo Bunge kushindwa kuisimamia serikali kikamilifu.

Pia kuna kitu kinaitwa kujiuzulu na kutishia kujiuzulu. Huko ni kwa kuandika barua ya kujiuzulu na kutangaza kujiuzulu kisha kupeleka barua kwa mamlaka ya uteuzi. Hicho ndicho alichokifanya Simai.

Kutishia kujiuzulu ni kuandika barua ya kujiuzulu kwa mamlaka yako ya uteuzi, kuomba ruhusa ya kujiuzulu. Ukikubaliwa ndipo unatangaza na wako viongozi wengi waemeandika barua hizi, lakini baadhi hazikukubaliwa, hivyo hawakujiuzulu, ndio maana nasisitiza hii 'boldness' iliyoonyeshwa na Simai, inapaswa ipongezwe na iwe ya kupigiwa mfano. Badala ya kusakamwa, kusimangwa na kukaliwa vikao, Simai apewe maua yake!

**Wasalaam**
**Paskali 0754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Wapinzani msipoangalia Chifu Bagalole atakufilisini



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KWA kawaida katika familia zetu kukiwa na mtoto mwenye matatizo pengine ya kujisaidia usiku kitandani, wazazi humfichia siri na kumkemea kimya kimya ili siri hiyo isitoke nje kwa kuwa itakuwa kero kwake.

Lakini kwa majirani, kwa mfano, endapo familia husika inajiweza na kukatokea dosari kama hiyo, majirani wakiipata hujitahidi kuisambaza ili angalau kuidhoofisha kisaikolojia.

Hata hivyo, inakuwa vigumu sana majirani kuaminiwa kwa kauli zao dhidi ya mtoto huyo au familia hiyo yenye ukwasi kama ambavyo familia yenyewe ya mtoto itakavyoitoa siri hiyo itaaminika. Kwa kufanya hivyo, itakuwa imetoka kwenye 'kinywa cha farasi'.

Ukijiweka kwenye muktadha wa kisiasa ambamo kuna mfumo wa vyama vingi vya siasa, mambo huwa kama hivyo kwamba chama kimoja kinajitahidi kuficha siri yake ili isitumike kukibomoa.

Chama tawala au uongozi kitajitahidi siku zote kuonyesha mema kinayofanya na kuficha mabaya yake. Hali kadhalika, chama cha upinzani nacho kitafanya hivyo ili kuvutia wapigakura.

Nikimtazama Chifu Bagolole namwona kabisa akiakisi hali hiyo katika siasa za nchi hii kwani katika ziara yake ya 'Back2Back', kinachomtoka kinywani, akihutubia wananchi 'wanaomkimbilia' hakika ni kizito na kinafikirisha.

Chifu Bagolole ameamua liwalo na liwe na kama kufa bado hajafikia wakati huo na kama kurogwa endeleeni kuchezea manyanga na vibuyu lakini yeye anaendelea kuimarika na kupambania wanyonge.

Chifu huyo wa Kisukuma, amebaini kuwa kazi anayofanya ndiyo hasa inatakiwa, akiita wananchi majukwaani wakianika kero na kadhia zao na yeye kuzitafutia ufumbuzi sawia, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha kwa baadhi ya watu.

Ameshuhudiwa akijitosa kusaidia wananchi wenye matatizo, huku Chifu Hangaya akimwunga mkono na kuongeza msaada pale anapokuwa ameanzia na kuishia Chifu Bagolole, na wakati mwingine humpandia hewani kumpongeza kwa anayofanya.

Kaniacha hoi, juzikati alipoonekana wazi kuchoshwa na mizengwe na kuwatolea uvivu viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri, ambao alisema hawatoki ofisini, wakijikalia kama miunguwatu badala ya kusaidia wananchi.

Akaenda mbali na kusema watu hao wamekuwa wakijitokeza kwenye mikutano ya Chifu Hangaya na kuhanikiza kuwa hakuna mwingine kama yeye anaupiga mwingi, anatoa mabilioni ya fedha za miradi lakini kumbe ni kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa.

Akafika mahali akamwunga mkono kinamna Chifu Kigwa ambaye amekuwa akibainisha kuwapo baadhi ya mawaziri waliojilimbikizia mali, wakinunua makasri Ugahaibuni na Bongo pamoja na magari ya kifahari huku wakiongoza mafukara pangu pakavu tia mchuzi.

Aliponiacha hoi zaidi, ni alipose‌ma akishamaliza 'Back2Back' tu, ataanika hadharani kila kitu, ikiwa ni pamoja na hao wanaojifanya kuwa karibu na Chifu Hangaya kumbe wakimng'ong'a na kumzunguka mbuyu. Siku hiyo walahi patachimbika!

Hii itatukumbusha Septemba 2007 pale Mwembe Yanga, Temeke, siku Dk. Willibrod Slaa aliposimama jukwaani na kutoa orodha ya aliowaita mafisadi wa nchi hii, akiorodhesha vigogo 10 na kutikisa nchi.

Sijui siku hiyo Chifu Bagolole atasimama jukwaa la mkoa gani kuhanikiza watu hao ambao nina uhakika watajisikia vibaya na kama wangeota, bora wangemwagia manyanga kabla ya kukutwa na 'siku ya Bagolole'.

Lakini kwa kinachoendelea ni kana kwamba Chifu Bagolole anafanya kazi ya upinzani kwa kueleza kinachotokea upande wa serikali ya chama tawala, husus‌an udhaifu uliomo unaopaswa kutumiwa na upinzani kujizolea kura.

Chifu anaweza akashangiliwa na wa chama chake kwa anachokifanya lakini wajiandae kwa matokeo kwani sasa inaonekana hakuna kinachofanywa na watendaji kwa wananchi wanyonge na ndiyo sababu wanamkimbilia Chifu kusaidiwa.

Pamoja na hayo, Chifu Bagalole anayeonekana kufuata nyayo za 'Jiwe' akipita huku na huko na kutoa fedha kusaidia watu, huku Chifu Hangaya naye akimsaidia, ni dhahiri wenye matatizo ni wengi lakini watu watajiuliza, kwa nini wanaosaidiwa ni wanaolalamika mikutanoni tu?

Hakika kwa 'Back2Back' hii, upinzani usipoangalia, hautakuwa na kazi ya kufanya kwani anachokifanya Chifu Bagalole ndicho ulipaswa kufanya wakati huu, vinginevyo muda ukiwadia, utakuwa unaishi kwenye nadharia zaidi.

Inawezekana ni mbinu ya chama tawala kupoka wapinzani donge kinywani ili wakose cha kutafuna wakati huu na wakati ujao, hususan nyakati za uchaguzi kwani walichotaka kukitumia kama silaha, tayari Chifu Bagalole ameshakianika na kufanyiwa kazi.

Piga kazi Chifu Bagalole usiogope kufa kwani 'role model' wako Magu, alipiga kazi na akaumaliza mwendo na amepumzika peponi. Tunasubiri siku ya 'List of Shame' kama si pale Mwembe Yanga, basi hata Chato!

## Mkandarasi mradi maji aingia mitini

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MRADI wa uchimbaji visima 11 unaogharimu Sh.milioni 363.3 katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida umekwama baada ya mkandarasi aliyepewa zabuni hiyo kukimbia, huku akiwa ameshalipwa Sh.milioni 73.

Hayo yamebainika juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni baada ya Kaimu Meneja Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Bernard Marcely akijibu maswali ya madiwani.

Madiwani hao walihoji kutokamilika kwa miradi ya kuchimba visima kwenye kata zao.

Marcely alisema kulingana na mkataba Kampuni ya Coyesa Co.Ltd ilipewa zabuni ya kuchimba visima 11 wilayani Manyoni kwa gharama ya Sh.milioni 363.3 kazi ambayo ilitakiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Alisema mkandarasi huyo tangu apewe kazi hiyo na kulipwa Sh.milioni 73 amechimba visima vitano ambavyo vinatoa maji katika vijiji vya Mbwasa, Majiri, Igwamalete na Makasuku ambapo baada ya hapo ameingia mitini na hajulikani alipo.

"Mkandarasi huyu kila tukimpigia simu aje kwenye kikao haji na hajaonekana 'site' tangu Novemba 2023 na kimsingi Sh.milioni 73 alizolipwa ambazo zinatolewa na Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) ambao upo chini ya Wizara ya Maji hazilingani na kazi aliyoifanya," alisema.

Marcely alisema kutokana na ukaidi wa mkandarasi huyo RUWASA imeanza mchakato wa kuvunja mkataba na kutafuta mkandarasi mwingine ambaye atafanya kazi ya kuchimba visima sita vilivyobaki.

Baada ya maelezo hayo, madiwani waliitaka RUWASA kuvielekeza Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSO) kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya maji kwa jamii.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mlagaza, alisema endapo CBWSOs hazitajenga utamaduni wa kutoa taarifa ya mapato na matumizi basi miradi ya maji inaweza kufa kutokana na usimamizi na matumizi mabaya ya fedha za maji.

Hata hivyo, Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Manyoni, Marcely alisema baadhi ya CBWSOs hazifuati maelekezo lakini ofisi ya RUWASA inaen-

# Gwajima aonya watoto kulala na simu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi na walezi kutoruhusu watoto kulala na simu na kutumia vifaa vya kielektroniki chini ya uangalizi ili kuwalinda na ukatili wa mtandaoni.

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye uzinduzi wa kampeni mahsusi ya ulinzi na usalama wa watoto mtandaoni itakayotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari 2024 hadi Januari 2025 na hatimaye kutoa nafasi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wake.

"Mtoto asiruhusiwe kwenda kulala na simu, anaweza kuwa anakesha ukifikiri amelala; ni hatari kwa usalama na afya yake, wazazi hakikisha mtoto anatumia vifaa vya kielektroniki akiwa chini ya uangalizi wa karibu ili kutojiingiza katika mitandao ambayo ni hatari kwa usalama wa mtoto," alisema.

Waziri Gwajima aliwaasa wazazi au walezi kuweka kiwango cha muda wa matumizi ya vifaa vya kieletroniki hasa luninga ili kukwepa janga la urahibu na kutoa muda kwa mtoto kufanya kazi za nyumbani ikiwa pamoja na kujisomea.

"Wazazi au walezi, waruhusuni watoto kushiriki katika majukwaa yao yaani mabaraza ya watoto shuleni na madawati ya ulinzi wa watoto ili kujengeana uwezo kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu ikiwa pamoja na namna ya kubaki salama katika mitandao. Majukwaa haya yapo chini ya uangalizi wa walimu wa malezi,"alisema.

Dk. Gwajima alisema matumizi ya mitandao yanaweza kuwaunganisha na watu wanaowajua na wasiowajua ambao hawana nia njema wakawadhuru kiakili au kimwili.

Alifafanua kuwa utafiti uliyofanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la UNICEF mwaka 2022 kwa watoto wa Tanzania wa umri wa miaka 12 hadi 17 ulibainisha kwamba asilimia 67 ya watoto wanatumia mitandao.

Alisema mitandao maarufu inayotumiwa na watoto ni pamoja na facebook, twitter, Instagram, whatsapp, tiktok na telegram.

Aidha alisema asilimia tano ya watoto waliotumia mitandao walishawishiwa au kulazimishwa kwa vitisho kutuma picha zao za utupu. Alisema pamoja na faida nyingi za mitandao zinazowakuta watoto katika matumizi ya mitandao bila uangalizi wa karibu zinajumuisha kuanza ngono katika umri mdogo, athari za kisaikolojia na mmonyoko wa maadili unaotokana na mwingiliano wa mila na desturi za mataifa mengine ikiwa pamoja na ushoga na usagaji.

Naye, Naibu Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew alisema teknolojia inakuja kama upepo huwezi kuzuia kinachotakiwa hivyo kinachotakiwa ni kwenda nayo na kutoa misingi ya kuibadili kwa faida ya Watanzania badala ya kuwa hatari.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq alisema suala la ukatili kwa watoto mitandaoni ni kubwa huku akiishauri wizara kuhakikisha wanatupia jicho.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema matukio ya ukatili wa watoto yamepungua kutoka 4,680 mwaka 2022 hadi 3,676 kwa mwaka 2023.

Alisema kwa mwaka 2023, watuhumiwa sita wa ubakaji na ulawiti kutoka Wilaya za Chemba, Kondoa na Dodoma Jiji walishtakiwa na kuhukumiwa ambapo watu wanne walihukumiwa miaka 30 na watu wawili walihukumiwa kifungo cha maisha.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Watoto Tanzania, Raphael Mayunga alisema wanaomba kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan ili awasaidie masuala ya kisheria ikiwamo uendeshaji wa kesi zinazowahusu.

Alisema ukatili wa watoto mtandaoni kwa kiasi kikubwa inatokana na kukua kwa teknolojia na kwamba wenye miaka 12 hadi 17 wanatumia mtandao bila uangalizi wa wazazi.



Kaimu Mkuu Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Benki ya Diamond Trust (DTB), Jesca Tugara (kushoto), akiuliza maswali kuhusu fani ya sayansi kwa mmoja wa wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa Shule ya Sekondari ya Alpha ya Kunduchi, wakati wafanyakazi kitengo cha Tehama cha benki hiyo, walipoadhimisha siku ya kimataifa ya wanawake na wasichana katika sayansi, shuleni hapo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MARY KADOKE**

# Ardhi watakiwa kutokuwa chanzo migogoro

**Na Munir Shemweta**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anthony Sanga, amewataka watumishi wa ardhi kutokuwa chanzo cha migogoro ya ardhi na badala yake wawe wasuluhishi.

Amewataka watumishi wa sekta hiyo kufanya kazi kwa uadilifu na weledi katika kutimiza majukumu yao, bila kusahau kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu.

Alitoa wito huo juzi mkoani Tabora alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua utendaji wa sekta ya ardhi pamoja na kuzungumza na watumishi wa sekta ya ardhi mkoani hapa.

Vile vile alikagua miradi inayotekelezwa na Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) pamoja na kujadili matatizo yanayoikabili chuo hicho.

Pia aliwaasa watumishi hao wa sekta ya ardhi kuhakikisha kuwa wanatoa majibu yenye uhakika kwa wateja na siyo kuwazungusha pale wanapohitaji huduma za ardhi.

"Mhakikishe mnatoa majawabu ya uhakika kwa wananchi badala ya kuwapiga danadana na kuwazungusha bila sababu. Mwananchi ajisikie kuwa kuhudumiwa vizuri katika sekta ya ardhi siyo anasa bali ni haki yake," alisema.

Aidha, aliwataka watumishi hao kujenga tabia ya kuonyana wenyewe kwa wenyewe pindi mmoja wao anapokwenda kinyume na kanuni za utumishi wa umma.

Akizungumzia suala la kodi ya ardhi, Sanga alisisitiza suala la ukusanyaji mapato kupitia kodi ya pango la ardhi na kuwataka makamishna wa ardhi wasaidizi kote nchini kulisimamia jambo hilo kikamilifu kwa kuweka mikakati madhubuti.

Pia aliutaka uongozi wa ARITA kutafakari ni namna gani watakuja na mipango ya maboresho ya kimitaala na miundombinu ya chuo, ili kiweze kujiendesha katika hali ya ushindani na vyuo vingine.

Alisema ataunda timu ndogo itakayokuwa na jukumu la kukaa na kutafakari na hatimaye kuja na mapendekezo ya kuboresha chuo hicho.


# MAISHA

Februari 11 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana


*Jumapili*





# NYUSI, KOPE ZINAVYOITA

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| K | ■ | N | D | E | G | E |
| U | ■ | ■ | ■ | L | ■ | N |
| N | ■ | M | K | E | ■ | D |
| G | I | A | ■ | Z | E | E |
| U | ■ | M | B | A | ■ | S |
| R | ■ | B | ■ | ■ | ■ | H |
| U | T | O | R | O | ■ | A |

## AMSHA AKILI


JAZA MAJINA YA MATUNDA UYAONAYO KATIKA VISANDUKU VILIVYOWAZI.



## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

NAO, TII, ZNZ, MTI, IGIZO, TINGA, IBANE, NDIZI, IGIZANA, SHIMONI

## WATOTO

# PAKA RANGI






Alichokifanya daktari

WATOTO wawili Juma na John walikuwa wanatembea pembeni ya bustani nzuri ya shule. Wakati wakipiga hatua waliona kipepeo akiruka ruka kwenye maua.Alipomuona kipepeo John alifurahi sana alianza kumuuliza Juma

John: Eti kipepeo ana rangi ngapi?

Juma: Huwezi kuhesabu kwani wapo wengi.

John: Wengi kama kiasi gani?

Juma: Huwezi kukisia kwa sababu ni wengi.

John: Kwa hiyo ukihesabu huwezi kumaliza?

Juma: Kamuulize mwalimu mimi na wewe bado wanafunzi

**SWALI**

Kisiwa cha Pemba kinasifika kwa kilimo cha zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Wajua kwa nini ndoa nyingi zinavunjika?

KARIBU msomaji tuzungumzie kidogo suala la talaka kama lilivyojadiliwa na baadhi ya wadau niliokutana nao kwenye kikao kimoja cha maandalizi ya harusi hivi majuzi. Wanasema ingawa ndoa nyingi zinafungwa karibu kila wiki, zingine zimevunjika baada ya muda mfupi. Ni kwa nini?

Ziko sababu mbalimbali zinazochangia ongezeko la talaka pamoja na ukweli kwamba ndoa zingine zimefanyika kwa gharama kubwa sana. Ziko zinazoanzia shilingi laki tano hadi milioni 15 na pengine zaidi kwa hapa kwetu. Ulaya huko ndiyo usiseme kwani huwa kufuru kutegemeana na uwezo wa familia husika.

Naam. Ndoa ni furaha, ndoa ni maridhiano kati ya mke na mume. Liko swali lilijitokeza wakati tunazungumza na jamaa fulani waliojumuika katika kikao kile cha harusi. Kwa nini mke na mume huachana baada ya kuwa wamejenga uhusiano kwa muda mrefu hata kufikia kufunga pingu za maisha?

Jibu ya swali hili ni pana sana. Msomaji wangu, nitajaribu kulijibu kupitia maeneo machache tuliyojadili kwa muda mfupi wakati wa mazungumzo yale. Moja ya sababu zilizotajwa ni tatizo la kiuchumi.

Tatizo hilo nililianzishia mjadala mimi. Nikasema kwamba zipo ndoa ambazo ama huvunjia au wanandoa kutengana kama siyo kuachana kabisa kutokana na uchumi wa familia kuyumba.

Mwanamke anaweza kuolewa na mwanaume tajiri na maisha yakawa murua. Lakini kama ambavyo uchumi wa nchi au wa dunia unavyoweza kupata misukosuko kama tunavyoshuhudia nchi mbalimbali, pia uchumi wa familia unaweza kuyumba.

Inapotokea uchumi wa familia unayumba, kwa kipato cha baba au cha mama kupungua, familia ya aina hii iliyozoea maisha ya kifahari, hapo ndipo mitafaruku huanzia.

Hali hii haizikumbi familia tajiri tu bali hata zile za kawaida. Jamaa anafanya biashara ndogo ndogo. Wakati mwingine mtaji hukata na hivyo huduma nyumbani kuleta wasiwasi. Milo mitatu inakuwa miwili na pengine mlo mmoja, ada inasumbua. Mama mmoja akadakiza;

"Umesema ukweli. Kuyumba kwa uchumi wa familia kumeleta shida sana katika baadhi ya familia. Kumechangia msongo wa mawazo kwa kinamama hata kuzikimbia kwa muda familia zao kama siyo kutokomea kabisa, hasa wale wasiofungwa na mkataba wa ndoa.

"Pamoja na ukweli huo, hiyo siyo sababu ya kutengana kwa sababu baba au mama wanapaswa kuwa ngangari kupambana na mtikisiko huo wa kiuchumi ndani ya familia", alisema mama huyo.

Baba mmoja aliyeshiriki mazungumzo hayo alisema, "huwa nawashangaa sana kinamama wanaokimbia nyumba zao au wanaofanya vitimbi baada ya kuona waume zao wanayumba kiuchumi".

Mama mwingine akachekesha pale aliposema; "Tuambizane ukweli, kama mumeo unajua kabisa ana uwezo kifedha, lakini huduma nyumbani ni 'mbofu mbofu', na wakati huo huo unapata uthibitisho kuwa anamjengea mwanamke wa pembezoni nyumba au kamnunulia gari, kwa nini usicharuke na hata ikiwezekana kubomoa ndoa? Si heri na mimi nikatafute anayenijali kuliko huyu niliyemvumilia kwa shida sasa kapata ananitosa?"

Mwingine aliyekuwa pembeni anafuatilia majadiliano yale akajisogeza karibu na kusema; "Niliomba talaka hata kabla ya kumaliza miaka miwili tokea tufunge ndoa ya nguvu na mume wangu. Ni pale nilipogundua kuwa mume yule alishaoa na kuacha wanawake wa nne na mimi ilikuwa ndoa ya tano. Hakunielewa kwa nini nilichukizwa kiasi kile."

Sababu zingine katika majadiliano yale ni unywaji wa pombe kupita kiasi hasa kwa mwanaume, hali inayoathiri huduma nyumbani kuanzia chakula na hata haki ya ndoa. Hali hiyo hufanya kinamama wengine hudai talaka ili wakajiridhishe kwingineko. Uaminifu unapotoweka ndani talaka hunyemelea.

Pia familia kugawanyika kikazi nako kumeelezwa kuchagia talaka. Baba anafanya kazi Dar na mkewe kahamishiwa ualimu Kigoma. Wawili hao ambao ndio kwanza wana watoto wawili, utengano huo kama siyo kuruhusu mahusiano mengine kwa mazingira waliyoko ni kitu gani? Hili nalo linatajwa kuwa ni tatizo linalotakiwa kutizamwa kwa macho mawili. Vinginevyo nyumba ndogo zitachipuka kila kukicha jambo ambalo ni hatari.

**Talaka siyo jambo lenye afya, kwani huchipua mengine kama vile kugombania mali za pamoja au kugombania watoto. Maisha Ndivyo Yalivyo. Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Ugomvi wa ndoa yenu, mtoto anahusikaje ubaya wa baba?

BINAFSI naamini zaidi katika falsafa moja ya kuwa elimu inaweza kuniweka huru katika fikra. Sitamani hata siku moja kuwaza kwa tumbo langu.

Naamini katika kuacha alama za kizalendo katika taifa langu. Katika dunia hii na zama hizi, ni vyema kujiuliza, sawa! Najivunia kwamba ninayaishi maisha ninayoishi sasa, nimejielimisha hata kama si kwa kiwango cha PhD (Shahada ya Udaktari wa Falsafa) lakini nina uwezo wa kuelimisha jamii yangu na kujifunza kutoka kwa mtu au watu wengine ili kupata maarifa zaidi.

Kama ndivyo! Tuishi kwa kuamini kuwa kuna mwanadamu anaweza kubaniwa sana fursa nyingine, lakini si uwezo wa kuelimika na kufikiri.

Ni sawa! Ngoja niwashirikishe jambo moja linalozitesa ndoa nyingi au uhusiano wa watu hivi sasa katika nchi yetu. Kuna wanawake hawaishi visa kama si kisirani. Nazungumza na wale ambao wanashirikishana matatizo yao ya ndoa na watoto wao. Tafadhali usifanye hivyo, mwache mtoto akue; huyo ni kiumbe asiye na hatia.

Inakuwaje maumivu yako ya uhusiano au ndoa unamweleza mtoto? Ooh mara nilipokuwa na mimba yako, baba yako alikuwa na mchepuko, alikuwa na Selina huko!

Mama! Acha hiyo habari kabisa. Unaharibu nafsi za watoto na unabeba laana. Waache watoto wakue wakimfahamu baba yao, kama baba yao na si mtu katili.

Ndugu yangu, zunguka mtaani kwako utawaona baadhi ya kinamama wako na watoto wao ambao wana makasiriko dhidi ya baba zao. Kiufupi hawasemezani, kisa hayo mambo mambo.

Watoto wameenda Ulaya, wako Marekani, wana kila kitu, basi simu zikipigwa mama anaongea saa tatu, halafu unasikia pale mwishoni msalimie dady (baba).

Wazazi wa kiume ukiwaona ni kama mabuldoza yanayotengeneza Barabara, inakuwa na lami nzuri, halafu ikishamaliza kazi, anayeliongoza anaambiwa hilo buldoza halitakiwi kupita tena kwenye hiyo barabara, litaharibu barabara.

Yaani hayo ndipo maisha ya wanaume waliotengenezewa shonde na wazazi wa kike kwa watoto. Tazama wanaume hawana umoja, maana ni wanyonge.

Hawana hata umoja wa wanaume, wafanye nini, wako tu. Lakini kimya kingi kina mshindo mkuu.

Ni vile haujui tu. Mara nyingine laana zinakuja kwenye familia kwa sababu ya mambo kama hayo.

Iko mifano hai huko mitaani tunakoishi, tunaona kuna familia watoto walikuwa juu, na baadae wamesambaratika wakaisha kabisa.

Hata ukiambiwa hii familia ilishawahi kufika katika hatua fulani ya kiuchumi, walikuwa na maisha mazuri, watu waliwachukulia kama 'role mode'l (mtu wa kupigiwa mfano), huwezi kuamini.

Na jambo zuri zaidi ni kwamba huyo baba wala halaani, lakini Mungu pia ni wa haki.

Kinamama wa aina hiyo wanaona sehemu ya kutua mizigo yao ni kwa watoto. Unaua familia na kuondoa umoja wa familia na kusababisha baba kukosa uthamani.

Kuna wanawake wana akili, hata kama baba hana kitu kabisa, mama amechukua mkopo, vikoba au kausha damu, halafu anamwambia mzee, hebu chukua hii, nenda kalipe ada ili watoto waone baba yao ndiye amelipa.

Sasa kutana na wale wanaoitwa 'ceremonial husbands' au l'uxurious husbands', hao ni wazee wa bata; hapa nazungumzia watu wawili tofauti. Mume anayejua majukumu yake, yaani 'responsible husband'.

Lakini usikutane na mume wa starehe (ceremonial husband), mume wa bata batani; ndo utajua kwa nini wanasaikolojia wanasema mwanamke anaongea maneno 36,000 kwa siku kutokana na msongo wa mawazo.

Wanawake wanaotoa pesa na kuwafutia aibu waume zao ili wasionekane hawana kitu au wanaume suruali; hao ni wale wanawake wenye akili zao, wanaojua kesho ya watoto wao.

Kwa wanawake wengine sasa ambao ni wale wanaotaka kuonekana ni staa saa zote, ni mimi tu, mkono mmoja, ungezaa mwenyewe tukuone, heshimu ndevu hata kama hazina pesa.

Ndugu yangu kwa haya yanayoendelea, mama kumjaza mwane sumu ili amchukie baba yake, kisa mgogoro wao wa mahusiano, amka ombea uzao wa kiume. Kama una mume, muombee mume wako sana. Kama una mtoto wa kiume, muombee sana.

Kama una kaka yako wa kiume, muombee sana maana roho la Yezebeli limeipindua dunia, tangu maamuzi ya mkutano wa Berlin mpaka leo, matatizo ya dunia hii ni makubwa sana kwenye masuala ya uzao kiume.

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**









Nderemo na vifijo vilisikika wakati Daud Chamwanga na Joyce Kuboja walipofunga pingu za maisha katika kanisa la Katoliki Ipuli, mkoani Tabora Februari 3, mwaka huu na baadae walijumuika na ndugu, jamaa na marafiki kwenye tafrija fupi ya kuwapongeza iliyofanyika kwenye ukumbi wa Citizen.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## GAUNI MABEGA WAZI

MAJIRA ya joto ni kipindi ambacho watu wanapenda kuvaa nguo nyepesi kwa ajili ya kuupoza mwili kutokana na hali mbaya ya hewa.

Baadhi ya wanawake wanapambana na hali ya joto kwa kuvaa nguo pana angalau kufanya miili yao kupumua na kuepukana na kutokwa na jasho kila wakati.

Hata hivyo, wataalamu wa mavazi wanasema njia bora ya kupambana na joto ni kuvaa magauni yanayotengenezwa kwa kitambaa cha pamba nyepesi, fupi kiasi na sehemu kubwa ya mabega yakiwa wazi.

Magauni haya ambayo ni rahisi kununua na kuyatuza, ni mazuri kwa wanawake wa rika zote.

Baadhi ya wabunifu wameongeza nakshi kwa kuweka maua na urembo mwingine shingoni na chini ya gauni ili kuyaongezea mvuto.

Kwa kunogesha zaidi sehemu ya kifuani unaweza kuweka kitambaa laini kwa ndani ili kuweka ulinzi pamoja na mkanda wa elastiki chini unaofanya umbo kugawanyika vyema.









UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# NYUSI, KOPE ZINAVYOITA

UREMBO wa mwanamke unaanzia kwenye sura, kutokana na ukweli kwamba eneo hilo linatafsiri uzuri na ustadi wake.

Kiungo cha kipekee ambacho kinasimama kama nguzo kwa uso ni nywele zinazoota juu ya macho zinazojulikana kama nyusi na kope ambazo zinapamba jicho.

Hata hivyo, mwanamke anakuwa mrembo zaidi kama akiwa na nyusi au kope ambazo ni za asili.

Nyusi na kope za asili hazina gharama za utunzaji au kuhatarisha usalama kutokana na uwepo wake.

Vitu vinavyotumika kwa ajili ya kutunzia nyusi za asili unaweza kuvinunua na kuwa navyo nyumbani hasa brashi la kupakia mascara.

Faida ya kutumia njia hii kukuza nyusi au kope zako ni kuwa na mwonekano mzuri kwa muda wote wa maisha yako.

Hatua za kufanya

Safisha vizuri brashi yako ili kuondoa weusi wa mascara.

Ukishasafisha hakikisha unakausha kwa kitambaa au taulo safi kabla ya kuanza kutumia.

Kama ulikua umepaka make-up au umepaka mafuta yoyote nawa ili uso wako uwe mkavu.

Chukua brashi yako na uiweke mafuta ya vaseline

na uanze kupaka kwenye nyusi zako au kope.

Fanya hivi kwa muda wa wiki na utaona matokeo unaweza kuendelea kufanya mpaka pale utakapo ridhishwa na urefu wa nyusi au kope zako.

Hakikisha unapaka mafuta hayo kwenye kope zako wakati wa usiku.







MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# TAMBI ZA MAYAI

LEO katika safu yetu ya mapishi tutaelezana namna ya kupika chakula rahisi zaidi aina ya tambi za mayai.

**MAHITAJI**

Tambi nusu paketi, vitunguu maji viwili vikubwa, karoti moja, hoho moja na vitunguu swaumu vilivyokatwa vipande vidogo kijiko kimoja cha chakula.

Mahitaji mengine ambayo siyo lazima ni carry powder kijiko kimoja cha chai, njegere zilizochemshwa nusu kikombe, mafuta kwa kiasi upendacho, mayai mawili na chumvi kwa ladha upendayo.

**NAMNA YA KUPIKA**

Chemsha maji ya moto yanayotokota, ongeza chumvi na mafuta kidogo, weka tambi kwenye maji hayo chemsha hadi ziive.

Baada ya kuiva epua na chuja maji yote ili kupata tambi kavu.

Ziweke kwenye bakuli pasua mayai kisha weka pembeni.

Chukua kikaango na weka mafuta, vitunguu maji, vitunguu swaumu, pilipili hoho, karoti na carry powder kisha kaanga kwa pamoja katika moto mdogo kwa muda mfupi kwani mboga hazitakiwi kuiva sana.

Ongeza tambi na njegere katika kikaango, geuza kila mara ili kuchanganya .

Weka mayai kwenye tambi kisha geuzageuza hadi mayai yaive na tambi ziwe kavu na zitakuwa tayari kwa kuliwa.

Ukitaka tambi zako zisivurugwe yaani ziwe kavu kama chipsi yai , ukiongeza mayai usizigeuze hadi unapoona yai limeiva kwa chini unageuza upande wa pili.

Furahia mlo wako wa mchana au usiku kwa kunywa na juisi, soda au chai.



MAISHA NI NYUMBA

## Meza 'console' inavyopamba nyumba



**Na Restuta James**

KUNA miezi hii ambayo watu wengi hawaipi uzito wa kuwepo ndani. Wengi wanazingatia kupata meza ya kulia chakula pamoja na ile ya kahawa (coffee table), ambayo mara nyingi huiweka sebuleni.

Leo ninakuletea meza ya console ambayo ina umuhimu wa kipekee ndani ya nyumba. Wataalam wa mapambo wanaieleza kama meza muhimu ya kuweka vitu 'adimu' na muhimu.

Wanaeleza kuwa ni meza inayoweza kutumika kuweka chetezo cha udi kwa wale wanaopenda marashi hayo na pia inafaa kwa matumizi ya mishumaa.

Hapa ndipo unapoweza kuona umuhimu wake. Wanaeleza kuwa si kila mahali chetezo inaweza kuwekwa; jambo ambalo halina ubishi.

Kwa wapenzi wa mishumaa yenye harufu nzuri, meza hii inawahusu sana. Wataalamu wanatukumbusha kwamba si kila mahali panafaa kuweka mishumaa hiyo.

Wanaeleza kuwa inaweza kuwekwa kwenye korido karibu kabisa na sebuleni au nyuma ya sofa kubwa kulingana na mpangilio wa sebule yako.

Kadhalika, inaweza kuwekwa karibu na sehemu ya kunawia mikono mnapolia chakula. Kwa kuwa ina matumizi maalum ya kuweka manukato, haipaswi kuwa mbali sana na maeneo hayo.

Hata hivyo, wanashauri kwamba meza hii inapaswa kuwa ndogo na ndefu wastani na pia inakishiwe kwa vitu vichache.

Inaweza kuwa na droo na inapendeza zaidi kama itakaa kwenye ukuta wenye kioo.

Wataalam wanatahadharisha kwamba kamwe meza hii haipaswi kuwa stoo ya kuhifadhia vitu. Isitumike kuweka madaftari au vitabu vya watoto.

Kama ni lazima sana basi unaweza kuweka jarida maridhawa unaloweza kupepesa macho pindi unawasha mshumaa au udi wako na si vinginevyo.

Pia inaweza kutumika kuweka picha nzuri moja tu ya familia au ya mtu mahsusi ili unapowasha mshumaa upate tabasamu. Pia inaweza kuweka ua dogo la asili au la kutengeneza.

Meza hii inatajwa kama sehemu inayoweza kumtambulisha mwenye nyumba kwa mgeni.

Kwa mujibu wa wataalam hao ni kwamba hii ni meza inayoeleza hisia za mwenye nyumba.

**Na Elizabeth Zaya**



# CHUKUA TAHADHARI KUIMARISHA USALAMA WA NYUMBA

USALAMA wa nyumba ni jambo la msingi kuliko vyote katika ustawi wake.

Mbali na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika nyumba kuanzia maandalizi, wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi ni pamoja na kuweka mfumo mzuri wa kuepusha majanga ya moto.

Erick Mahimila anasema ziko njia mbalimbali za kutumia kukabiliana na majanga ya moto kwenye nyumba na kwamba mojawapo ni kutumia mfumo bora wa umeme kwa kuwa mengi husababishwa na hitilafu zinazotokana na mifumo duni ya umeme kwa kuweka vifaa duni wakati wa kuweka umeme huo kwenye nyumba.

Njia ya pili anasema ni kutumia vizuri soketi na swichi ya umeme pamoja na kuepuka kutumia vifaa vya umeme duni ikiwamo redio, pasi, jokofu, televisheni, jiko na vinginevyo.

"Kutokana na ujenzi duni, si jambo la kustaajabisha kukuta nyumba moja ina soketi moja au mbili. Hili husababisha watu kujaza kila kifaa kwenye soketi hiyo moja, na kusababisha soketi hiyo izidiwe na kuwaka moto," anasema

Ya tatu anasema ni kutumia vema jiko lililoko ndani ya nyumba.

"Jiko lililoko ndani ya nyumba unatakiwa kuchukua tahadhari zaidi. Haijalishi ni jiko la umeme, gesi au mafuta unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ili kuepuka majanga ya moto. Lisafishe, usiliache likiwa na mafuta au kuacha karatasi karibu nalo," anabainisha huku akitaja njia ya nne kuwa ni kuepuka kuacha moto ukiwaka karibu na nyumba.

Anashauri pia kutumia moto ulio wazi kwa uangalifu na kwamba wakati mwingine watu huwasha vibatari, mishumaa au hata sigara ndani ya nyumba.

Kwamba ni vema kuandaa miundombinu na vitu vya kukabiliana na moto.

"Ni vema kuchukua tahadhari kabla ya janga kutokea, ni muhimu ukahakikisha nyumba yako ina miundombinu ya kukabili moto pamoja na vifaa vya kuzimia moto. Weka vifaa vya kuhisi moto au moshi.


"Hakikisha watu wanaweza kujiokoa kwa kupitia madirishani au kwenye milango ikiwa moto utatokea. Yaani jenga madirisha na milango inayoruhusu watu kujiokoa.Weka vifa vya kuzimia moto kama vile mpira wa maji wa kuzimia moto pamoja na mitungi ya hewa," anasema

Anashauri usitumie vitu vinavyoshika moto haraka ikiwamo mafuta ya gari, rangi, gesi, pamba.


Anasisitiza: "Hakikisha unachunguza kila bidhaa unayotaka kuiweka kwenye nyumba yako ili kubaini kama inashika moto haraka ili ihifadhiwe kwa tahadhari kubwa."

Lingine analoshauri ni kuchukua tahadhari umeme unapokatika kwa kuzima vifaa vya umeme.

Anashauri kutumia vifaa vya kutawala kiwango cha umeme, hivyo huhakikisha umeme unaoingia kwenye vifaa vyako ni wa kiwango kinachotakiwa na huwa na mfumo unaojulikana kama "delay" ambao hauruhusu umeme kuingia kwenye vifaa moja kwa moja mara unaporudi.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
ACHA KUNIPIGA SIASA, HAKUNA PESA ZA KULIPANA BAR.
UOGA TU. KULIPANA BAR KUNA FAIDA USIBISHE
KWANI KAKA HUJAWAHI KUSIKIA 'GEMU IMEAHIRISHWA' KUTOKANA NA SABABU KAMA HII TUNAYOIONA AU SIO KAKA'ANGU?
SIO KWA BIA ULIZO-NINYWEA
BONDENI
DUME ZIMA UGOMVI WA USIKU UNAKUJA NAO MPAKA MCHANA! LETE HELA YA KULA
TAFUTA NENO LAINI
ABIRIA JADILINI YANAYOWAHUSU, HAYO YAKUPIGWA VYETI DABODABO MUYAACHE.
USITUFUMBE MIDOMO WEWE ENDESHA GARI
MMEZIDI KUHARIBU SHERIA MBUZI NYIE!
SISI TUNGE-YAJUAJE?
EBANAEE! UTASHUKA USHAANZA KUTUITA MBUZI TUKI-KUCHEKEA UTATUKANA!
HII NI OFISI LAZIMA SISI WENYEWE TUJADILIANE LAKINI SIO NA NYIE ABIRIA
CHAKULA ULICHO-NIAGIZA UNATAKA KUWEKA 'STOKU' NYUMBANI KWAKO AU KUNITIBIA?
'NI MWIKO' KUHOJI MAAGIZO YA MIZIMU HATA UKIAGIZWA FUSO USIHOJI.
UMESHINDWA KUTUMIA CHIPSI MAYAI MSIMU HUU WA MVUA KUTATUA MGOGORO WA NDOA MPAKA UNATUMIA 'MAGUMI KWA MKEO?'
MPAKA NIMEKUWA MEMBA KWA WAUZA CHIPSI, LAKINI BADO "HAKIELEWEKI!"
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKITAKA KUJUA UMUHIMU WA JIRANI KAISHI MSITUNI...

## HABARI KIMATAIFA

# Netanyahu aamuru watu kuhamishwa mji wa Rafah

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAZIRI Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, amewaamuru wanajeshi kujiandaa kuwahamisha raia wa Kipalestina kutoka katika mji wa Rafah kusini mwa Gaza kabla ya mashambulizi makali hayajaanza.

Jumla ya Wapalestina milioni 1.5 wamekimbilia katika mji huo kutafuta hifadhi kutokana na mashambulizi kutoka vikosi vya Israel katika maeneo mengine ya Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, nchi ya Marekani imeionya Israel kuvamia mji huo na kuelezea itakuwa janga, huku Umoja wa Ulaya na Umoja wa Mataifa zikielezea wasiwasi kuhusu mashambulizi hayo.

Mashirika ya misaada yalisema kuwa haiwezekani kuhamisha kila mtu kutoka mjini humo.

Hata hivyo, Netanyahu aliwaambia maafisa wa kijeshi na usalama kuwasilisha kwenye baraza la mawaziri mpango wa pamoja wa kuwahamisha watu na ngome za Hama.

Ofisi ya waziri mkuu ilieleza jana kuwa haitawezekana kufikia lengo la vita bila ya kuwaondoa Hamas katika mji wa Rafah.

Ilisema taarifa hiyo kuwa kazi kubwa inahitajika kufanyika Rafah kwa kuwaondoa raia katika maeneo ya mapigano.

Mapema wiki hii, Netanyahu alisema amewaamuru wanajeshi kujitayarisha kufanya kazi ya kijeshi ndani ya Rafah na kwamba ushindi kamili wa Israel dhidi ya Hamas ulikuwa umesalia miezi michache kukamilika.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo baada ya kukataa masharti ya Hamas ya kusitisha mapigano.

BBC iliambiwa kwamba wajumbe wa upatanishi wa Hamas waliondoka katika mji mkuu wa Misri wa Cairo, huku mazungumzo kati ya pande hizo mbili yamesitishwa.

Wakati huo huo, hali imekuwa mbaya kwa watu wanaoishi katika maeneo ya kaskazini mwa Gaza baada kukumbwa na baa la njaa na kusababisha kula vyakula vya mifugo kujiokoa.

Watu wanaoishi eneo hilo waliambia BBC kwamba watoto wamekosa chakula kwa siku kadhaa baada ya serikali ya Israel kukataa kutoa vibali vya malori yenye misaada kuingia Gaza.

Baadhi ya watu wameamua kusaga chakula cha mifugo na kugeuza kuwa unga ili waendelee kuishi, hata hivyo akiba ya nafaka hizo imepungua.

Watu pia wameelezea kuwa wanachimba chini kwenye udongo ili kupata mabomba ya maji, ya kunywa na kusafishia.

Hivi karibuni Umoja wa Mataifa ulionya kwamba utapiamlo mkali miongoni mwa watoto wadogo kaskazini mwa Gaza umeongezeka kwa kasi na kufikia asilimia 15.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuratibu misaada ya kibinadamu, Ocha, lilisema zaidi ya nusu ya misheni ya misaada kaskazini mwa Gaza ilikataliwa kuingia hadi kufikia mwezi uliopita.

Katika taarifa yake ilisema kuna ongezeko la kuingiliwa na majeshi ya Israel kuamua wapi misaada hiyo itolewe.

Ilieleza watu 300,000 wanaokadiriwa kuishi katika maeneo ya kaskazini wamekatiwa msaada na kusababisha kukumbwa na njaa kali.

Msemaji wa shirika la kijeshi la Israel lililopewa jukumu la kuratibu upatikanaji wa misaada Ukanda wa Gaza, alisema katika kikao kifupi mwezi uliopita kwamba hakuna njaa katika eneo hilo.

**BBC**



Raia wa Kipalestina akisaka maji baada ya miundombinu ya usambazaji maji katika eneo la Gaza Kaskazini kuharibiwa na wanajeshi wa Israel. **PICHA: REUTERS**

# Wafuasi wa waziri aliyefungwa waongoza kwenye uchaguzi

**ISLAMABAD,** PAKISTAN

WAFUASI wa waziri mkuu wa zamani nchini Pakistan ambaye amefungwa jela, Imran Khan wanaongoza katika matokeo ya uchaguzi wa nchi hiyo kwa zaidi ya viti 100 vya bunge.

Kituo cha habari cha Geo News kilisema jana kwamba wagombea huru ambao wengi wao wanamuunga mkono Khan, wameshinda viti 47 kati ya 106 vilivyotangazwa.

Bunge la nchi hiyo lina viti 265 vilivyogombaniwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika Alhamis ya wiki hii.

Mpaka kufikia Ijumaa, Tume ya Uchaguzi ya Pakistan (ECP) ilitangaza matokeo rasmi ya viti 70 na kuwathibitisha wagombea hao huru wameshinda.

Chama cha Pakistan Peoples Party cha Bilawal Bhutto Zardari, mtoto wa waziri mkuu wa zamani aliyeuawa Benazir Bhutto, pia kilikuwa na viti 24 na chama cha Pakistan Muslim League-Nawaz cha waziri mkuu wa zamani, Nawaz Sharif, kilipata viti 18.

Khan yuko gerezani na chama chake cha Pakistan Tahreek-e-Insaf kilizuiwa kushiriki uchaguzi huo na kusababisha wafuasi wake washiriki kama wagombea binafsi.

**DW**

# Maandamano makubwa yaitishwa Senegal

**DAKAR,** SENEGAL

KAMBI ya upinzani nchini Senegal wameitisha maandamano kupinga hatua ya serikali ya kuahirisha uchaguzi uliopangwa kufanyika mwaka huu.

Maandamano hayo ni sehemu za jitihada za vyama vya upinzani kuonyesha nguvu zao dhidi ya Rais Macky Sall ambaye yuko madarakani.

Vikundi kadhaa vya kidini na kiraia na mashirika ya kitaaluma, ambayo yameungana katika vuguvugu hilo jipya, yametoa wito kwa watu kuhudhuria swala ya Ijumaa wakiwa wamevalia mavazi meupe na yenye rangi za taifa.

Wakazi wa mji mkuu wa Dakar, pia wamehimizwa kupitia mitandao ya kijamii, kuandamana kwenye uwanja mkubwa ulioko karibu na mji huo.

Hata hivyo, watu walioitisha maandamano hayo bado hawajajulikana, lakini wagombea wengi walioidhinishwa katika uchaguzi huo ulioahirishwa wametangaza wamepanga kujiunga na maandamano hayo.

Bunge la Senegal liliunga mkono uamuzi wa ghafla wa Sall kusogeza mbele uchaguzi uliopangwa kufanyika Februari 25, na kusababisha wapinzani kuwa na hasira kuhusu hatua hiyo.

**DW**

# Waziri wa ulinzi atembelea Goma

**GOMA,** DRC

WAZIRI wa Ulinzi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jean Pierre Bemba, amefanya ziara katika mji wa Goma katika hatua yake ya kutuliza wasiwasi wa wananchi.

Ziara yake hiyo aliifanya juzi wakati kuna hofu ya mji huo kutekwa na waasi wa M23 ambao wanapambana vikali na vikosi vya serikali.

Kwa mujibu wa waziri Bemba, alikuwa Goma kuwaona watu waliojeruhiwa kutokana na vita pamoja na kuzisaidia familia 12 zilizopoteza ndugu zao.

"Nipo hapa kutoa ujumbe wa faraja na kutoa msaada kwa rafiki zetu wanajeshi waliopo hapa wa SADC, makampuni binafsi ndugu zetu wazalendo,ambao nao wanapigana, tunawapongeza kwa ulinzi wa eneo letu " alisema waziri Bemba.

SAFU

MAKALA

# GHARAMA ZA VYAKULA HOSPITALINI ZIWE HALISI



Na Magabilo Masambu

**Akabadilisha gia angani, akasema" "Tunafanya hivyo ili pasiwapo na tofauti ya vyakula." Nikamuuliza wagonjwa wote wanafaa kula chakula cha aina moja yaani aliyefanyiwa upasuaji na anayeumwa mguu? Aah "unajua huu ni utaratibu wa hospitali". Nikamuuliza tena mbona gharama zinafanana kwa kila kinacholetwa halafu ni bei kubwa akasema yeye si msemaji! Nikamtakia jioni njema.**

LEO katika safu hii tuzungumze kidogo kuhusu suala la afya nchini. Kuna mambo kama serikali haitakuwa macho katika sekta ya afya, yatawaumiza sana wananchi. Bahati mbaya sana, serikali imekuwa na utamaduni wa kutazama zaidi taasisi zake kuliko kutupia macho zaidi taasisi binafsi.

Jambo la kwanza ni suala la wagonjwa kulazimishwa kula chakula cha hospitalini. Ni kweli kwamba mgonjwa kula chakula ni jambo jema katika kuimarisha afya yake anapokuwa anaendelea na matibabu au baada ya tiba. Hata hivyo, kulazimishwa huku kumekaa katika mtindo wa kibiashara zaidi kuliko kujali afya ya mgonjwa.

Kuna baadhi ya hospitali hasa za binafsi zinawalazimisha wagonjwa kula chakula cha gharama kubwa, ambacho hakiendani kabisa na gharama halisi. Mathalani, mgonjwa analetewa wali maharage sahani inauzwa Sh. 10,000. Analetewa bakuli mbili za mtori au vikombe viwili vya uji gharama zile zile. Kwa maana hiyo, mgonjwa kwa siku anatumia Sh. 30,000 mpaka 40,000.

Kibaya zaidi, kuna wakati mgonjwa hajisikii kula chakula kinachoandaliwa siku hiyo, lakini hospitali wanasema hakuna kingine ndicho hicho hicho. Unajiuliza hivi hapa tuko gerezani au hospitalini? Ukilazimisha kwamba ungehitaji chakula kingine, unaambiwa hospitali ina mgahawa, lakini kile kilicholetwa utakilipia hata kama hautakila. Kwa hiyo unalazimika kuingia gharama mara mbili.

Nikamuuliza mhudumu mmoja katika hospitali fulani kwa nini mnalazimisha wagonjwa kula chakula chenu tu tena kwa gharama kubwa? Jiibu alilolitoa ni kwamba: "Tunalinda afya za wagonjwa", nikamuuliza kwa hiyo ndugu walioamua kumleta mgonjwa wao hospitalini ni hatari zaidi kwake na kwamba wanaweza kumdhuru kwa chakula cha sumu au kichafu kama wangetaka kufanya hivyo wangemleta hospitalini?

Akabadilisha gia angani, akasema" "Tunafanya hivyo ili pasiwapo na tofauti ya vyakula." Nikamuuliza wagonjwa wote wanafaa kula chakula cha aina moja yaani aliyefanyiwa upasuaji na anayeumwa mguu? Aah "unajua huu ni utaratibu wa hospitali". Nikamuuliza tena mbona gharama zinafanana kwa kila kinacholetwa halafu ni bei kubwa akasema yeye si msemaji! Nikamtakia jioni njema.

Nachotaka kusema hapa ni kwamba tulinde uhai wa wagonjwa kwa kuwapunguzia mawazo wawapo hospitalini. Nasema hivi kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wengine wanachelewa kupona ama kupoteza maisha kabisa kwa kuwaza gharama za matibabu, pamoja na vyakula. Jambo la kuandaa chakula ni jema lakini gharama ziwe halisi na kama mgonjwa hajisikii kula chakula hicho, asilazimishwe kukilipia kwa sababu hakukitumia na hii ndiyo sababu ya paka wa hospitalini kunenepa kuliko kawaida.

Suala la afya linapaswa kuwa huduma, hivyo hatuwezi kusema iwe huduma moja kwa moja lakini kuwe na gharama za uchangiaji na si biashara. Wananchi wasio watumishi wa umma tunajua kazi kubwa wanayoifanya katika kulipa kodi nchini lakini wanapougua kwa sababu hawana bima za afya kama watumishi wa umma, wananunua afya zao kwa gharama kubwa.

Tufike mahali ambapo huduma za afya katika hospitali za umma na binafsi ziwe na ulinganifu ili mtu aamue aende wapi. Huduma katika hospitali za umma ziboreshwe zaidi. Jambo la kushangaza ni kwamba hata wenye dhama ya kuzisimamia nao hawatibiwi humo. Limekuwa kama jambo la shule tunajenga lakini watoto wetu wanasoma shule za binafsi, maana yake wanaoshindwa kulipia gharama binafsi wafe.

Nishauri pawepo na chombo maalum kama hakipo cha kuchunguza mwenendo wa gharama za matibabu kama ilivyo kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) barabarani. Si tu mtu anajiamulia kwa sababu hospitali ni yake anapanga gharama anazotaka na kwamba asiyeweza asije.

Yafanyike makubaliano na serikali kwa masharti kwamba serikali inakupatia hiki na kile, lakini gharama zako zisizidi hapa. Vinginevyo tunarudi kule kule wakati wa ukoloni, ambapo huduma zilitolewa kwa matabaka - mzungu, mwasia, na mwafrika. Tumepinga ubaguzi kisha tukaurudisha wenyewe.

Mwisho ni kuhusu rufani. Kuna baadhi ya hospitali wanang'ang'ania wagonjwa hata baada ya kuonekana wameshindwa kumtibu. Huu utaratibu unachangia kupoteza maisha ya Watanzania wengi. Kama mgonjwa kashindikana, mpeni rufani ya kwenda kwingine wala hautakuwa udhaifu wa madaktari na hospitali kwa ujumla.

Kuna wakati ndugu wa mgonjwa wanaona wazi kwamba mgonjwa wao hapo hatopona, wenye ujasiri wanasema "Jamani tunaomba mtuandikie rufani tutazame na kwingine" nalo linakuwa tatizo. Daktari anaingia huku anatokea kule mara kuna vikao mambo kibao, mpaka wakiona mgonjwa amekuwa na hali mbaya wanaanza kuhangaika na 'ambulance' kukimbiza mgonjwa mpaka wengine wanafia njiani.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Binadamu hatosheki, ukimpa tano leo kesho anataka kumi*



Na Adam Fungamwango

**"Atatokesha na nini eee, kweli binadamu hatosheki, kupenda hiki na kile, haoni raha moyoni kulalamika hachoki ee wakati anavutiwa ee, na kila kitu moyoni ee, binadamu hatosheki. Kwa vipi atatulia jamani, ikiwa apatapo hakitoshi, awe ni mwenye mali ataka tena kingine kwa tamaa aliyonayo ee tumwite nani huyu, wakati anavutiwa eee, na kila kitu moyoni, tumwite nani huyu eee binadamu hatosheki.**

MSANII Jay Moe aliwahi kutoa ngoma yake aliyoiita 'Jua na Mvua.' Anawauliza watu jua na mvua wanapenda nini? Wengine wanataka jua, na wapo wanaotaka mvua.

Kila mmoja anataka kitu kimoja kwa sababu zake. Mfano muuza kahawa na mahindi ya kuchoma watataka mvua kwa sababu biashara zao zitauzika sana.

Dobi atataka jua ili afue nguo za wateja wake, mvua kwake ni tatizo. Hapo utaona kila mtu anavutia kwake. Lakini hao hao kesho na kesho kutwa hali inabadilika.

Binadamu hajawahi kutosheka na kitu kimoja. Jua likiwaka mwezi mzima atalalamika na kusema joto limezidi bora ije mvua.

Itakuja baridi atafurahi siku moja tu na kusema 'bora joto' limepungua, lakini kesho tu, ataanza kulalamika.

Atajikunyata na kuvaa masweta, akisema baridi limekuwa kali sana na limemchosha.

Itakuja mvua, nayo atafurahi siku moja tu, kesho yake ataanza kulalamika kuwa inawafanya asifanye kazi zake kwa uhuru na inamharibia mipango yake ya pesa.

Huyo ndiye binadamu, hajawahi kuridhika na kitu kimoja. Mtu ana mke wa ndoa, lakini anatoka kwenda kutembea na michepuko nje.

Akila ugali wiki nzima, ataanza kusema ugali umemchosha, atataka wali. Huo wali nao akifululiza atasema umemkinahi.

Binadamu wengi wana tabia ya kupenda nyama. Lakini nayo akifululiza siku nne tano ataikataa na kusema imemkifu. Atataka kubadilisha mboga, hasa mboga za majani. Siku mbili au tatu tu atasema hazitaki tena zimemchosha. Hakuna chochote ambacho binadamu anatosheka nacho.

Ukimpa kitu chochote kidogo leo, kesho atataka aongezwe. Ndiyo maana mwanamuziki Tshimanga Kalala Assosa, akiwa na bendi ya Orchestra Makassy alifanya utafiti zake mdogo akagundua kitu hiki, akaja na wimbo wake alioupa jina hilo hilo la 'Binadamu Hatosheki.'

Assosa, mwanamuziki wa zamani wa Orchesta Bella Bella, Lipua Lipua, na Les Kamale, aliingia nchini mwishoni mwa miaka ya 1970 na bendi ya Orchestra Fuka Fuka iliyoundwa baada ya kujitenga na Les Kamale. Ilifanya ziada nchini Tanzania na ikawa na maskani yake maeneo ya Mlimani Park, njia ya kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kwa kiasi kikubwa bendi hiyo ndiyo iliyosababishwa kuundwa na Orchestra Mlimani Park, kwani baada ya kumaliza mkataba wake, waliowaleta hawakutaka tena kuwaongeza mkataba, badala yake wakaongea na wanamuziki wa Dar International kuhusu uwezekano wa kuunda bendi itakayokuwa na maskani yake hapo.

Asilimia 90 ya wanamuziki wa Dar Intenational ndiyo waliounda bendi hiyo iliyokuwa na mtindo wa Sikinde Ngoma ya Ukae mwaka 1978, wakaongezwa wachache kutoka Juwata Jazz Band, 'Msondo Ngoma', na Assosa aliyekuwa katika bendi ya Fuka Fuka naye akaongezwa.

Ndiye aliyetunga wimbo wa 'Naomba Usisamehe Gama', ingawa aliondoka mapema tu kabla haujarekodiwa. Aliyeuimba wakati wa kuurekodi ni Coamas Thobias Chidumule.

Assosa akajiunga na Orchesta Makassy mpya ya mwaka 1981, baada ya ile ya kwanza ya kina Dk. Remmy Ongalla ya mwaka 1978 mpaka 1979.

Ikumbukwe kuwa Mzee Makassy aliuza vyombo mwaka 1979, akaenda zake Ulaya na akarejea mwaka 1981 na vyombo vipya aina ya Ranger na kuunda upya bendi yake. Wakati huo Remmy alikuwa ameshajiunga na Super Matimila.

Ndipo alipomchukua Assosa aliyetunga wimbo huo, ukiwa ni moja ya nyimbo za mwanzo za bendi hiyo. Haya ndiyo mashairi ya wimbo huo.

"Atatokesha na nini eee, kweli binadamu hatosheki, kupenda hiki na kile, haoni raha moyoni kulalamika hachoki ee wakati anavutiwa ee, na kila kitu moyoni ee, binadamu hatosheki. Kwa vipi atatulia jamani, ikiwa apatapo hakitoshi, awe ni mwenye mali ataka tena kingine kwa tamaa aliyonayo ee tumwite nani huyu, wakati anavutiwa eee, na kila kitu moyoni, tumwite nani huyu eee binadamu hatosheki.

"Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika.

Hata ukimpa nini milele hataridhika ooo. Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika.

"Ukimpa tano leo, kesho anataka kumi.

Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika.

Leo jua limewaka binadamu achukia eee.

"Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika.

Kesho mvua inanyesha, hachoki kulalamika eee. Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika

Hata ukimpa nini milele hataridhika ooo. Eeee jamani mwanadamu hatosheki, hata ukimpa nini milele hatoridhika."

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

SAMAHANI dada kama nakufananisha!" Sauda alisikia sauti nyuma yake. Akawa anajiuliza ni nani anayemfananisha huku sokoni. Akageuka na kukutana na sura ya dada mmoja ambaye ni kama aliwahi kumwona sehemu fulani lakini hakumbuki. Yeye hakutaka kumwambia kuwa kama aliwahi kumuona sehmu fulani, akabaki kumtazama tu ili ajitambulishe.

"Wewe ndiyo mke wa Kassim eee?" Sauda alisita kidogo kwa sababu hakujua lengo la dada huyo ni nini, lakini kuna kitu kikamwambia hakuna baya, akubali.

"Ndiyo mimi!"

"Ooh vizuri, mimi ndiyo yule dada aliyekuja wiki ilee pale nyumbani kwenu, nilimfuata wifi yako tukaenda vikobani. Naitwa Fatuma."

Hapo ndipo Sauda alipofunguka macho, akikiri ni kweli kabisa ndiye yeye. Na ndiyo maana akili yake ilimwambia kuwa mtu huyu ameshawahi kumuona mahali.

"Ahaaa kweli, nimeshakutambua."

"Siku ile mwenzangu nilikuwa nimeupara mwenyewe nakwenda vikobani, leo nina kidela changu hiki cha kuendea sokoni, ndiyo maana umenisahau." Nusura Sauda acheke, lakini akajizuia.

"Vipi umekuja kununua mboga?"

"Ndiyo nimekuja kununua samaki wabichi, ila bei sasa, halafu wanapunja, wakakata vipande hidogo."

"Sasa kaka yangu leo unakwenda kumlisha mboga gani?"

"Nimenunua hivyo hivyo, na nazi hapo, nyanya chungu, bamia na mboga za majani, basi siku imeenda."

"Enhee dada, hebu niambie wifi yangu, siku ile nilipokuja kwenu kuna hali niliikuta nikaishangaa. Mnaishi vipi na wifi yako, maana yale maneno na ule uitaji unajua sikuupenda mimi, nusu nimjibu mimi..."

"We acha tu dada yangu, makubwa, madogo yana nafuu. Nateseka dada mle ndani, mume wangu tu ndiyo ananifariji na kunisihi nivumilie."

Sauda hakuwa na wasiwasi kwamba maneno atakayozungumza yatafika kwa wifi yake kwa sababu hata siku ile wakati anaamriwa kama mtoto mdogo, aliona sura ya dada yule ikibadilika na kuonyesha kutofurahiwa, na baadaye akatikisa kichwa kwa masikitiko bila Havijawa kuona kitu.

Na hiyo ndiyo iliyofanya hata alipojitambulisha, Sauda alionekana kumchangamkia, kwani ilionyesha kabisa siku ile alikuwa upande wake, japo hakusema kitu chochote.




**Sauda hakuwa na wasiwasi kwamba maneno atakayozungumza yatafika kwa wifi yake kwa sababu hata siku ile wakati anaamriwa kama mtoto mdogo, aliona sura ya dada yule ikibadilika na kuonyesha kutofurahiwa, na baadaye akatikisa kichwa kwa masikitiko bila Havijawa kuona kitu.**

"Hebu tukae pembeni kwanza huku unisimulie vizuri, maana hili jambo si la mwanamke mmoja, linaweza kumpata yoyote yule."

Hakumficha kitu, Sauda alimsimulia Fatuma kila kitu. Visa vyote alivyofanyiwa tangu alipoolewa, kuanzia alipoolewa. Hakuacha kitu. Fatuma alisikitika.

"Pole sana wifi yangu, yaani mtu anakuja hadi kuchafua ulipopiga deki! Anakuja kurudisha uchafu wa majani uwanjani ulipofagia. Huyo si mtu mzuri. Mimi kile nilichokiona siku ile tu ilitosha kufahamu kuwa wifi yako si mtu mzuri.

Sasa ni nikwambie shoga yangu. Umemlegezee. Ukimlegezea atakuona mjinga. Siyo umtukane hapana. Sehemu ambayo siyo usikae kimya na kumsubiri mumeo. Mwambie hili hapana."

"Kweli eeee!"

"Oooh, mimi si nakwambia, vinginevyo ataendelea kukufanya kama mtumwa, maana hata afadhali ya hausigeli."

Maneno ya Fatuma ambaye ni shoga wa wifi yake, aliyafananisha kabisa na shoga yake mwenyewe Paulina alivyomwambia siku za nyuma. Akili ikamrejesha nyuma na kukumbuna nasaha za shoga yake kipenzi.

"Sauda weee shoga yangu, yaani wifi ndiye anayekufanya unyorodoke hivyo? Umeisha umebaki mabega juu kama umetundikwa kwenye mti.

Usimwogope Sauda, sisemi kama umpige, au mpigane, lakini usiwe mnyonge, akikubwatukia na yeye mbwatukie, atakuogopa. Usimuendekeze.

Hutoona raha ya ndoa na ipo siku utaamua tu kufungasha virago urudi nyumbani. Pigania ndoa yako! Ndoa inakufa kwa nyinyi wenyewe wapenzi kugombana na siyo kwa sababu ya mtu mwingine ya pembeni, huo ni uzembe Sauda.

"Inawezekana wifi yako anakufanyia visa ili ukasirike uondoke. Inawezekana kuna msichana shoga yake anataka kumtengenezea nafasi, usichoke, ndoa yako bado changa sana rafiki yangu.

"Na hivi bado, yaani atakutengenezea visa ili mradi umchukie mumeo uondoke, usiruhusu hicho kitu. Usimchukie mumeo kwa sababu ya kikaragosi kimoja."

Aliyasikia maneno ya Paulina yakijirudia nyuma ya ubongo wake siku ile alipomtembelea kwake. Anachorudia Fatuma ndiyo hicho hicho. Ni kama vile tu wanafahamiana na wameambizana.

"Nilikutana na mumeo majuzi, nikamweleza yote niliyoyaona. Mwishoni nikamwambia ushauri anao mwenyewe, kusuka au kunyoa. Akae na dada yake amseme."

"Bora mwenzangu, unajua kwa sababu wewe ni rafiki ya dada yake atashtuka na kuona kweli kuna tatizo kubwa."

"Basi mwali wangu, wala usiwe na wasiwasi, litaisha tu hili utabaki salama na ndoa yako."

"Nashukuru sana."

"Ila usimwambie lolote kuhusu kukutana kwetu."

"Walaaa!"

**************************************

"Wee cha uvivu hebu amka huko! Mwanamke gani kaka yangu anaondoka asubuhi hata humpikii chai. We wa wapi wewe. Wazazi wako wamekufundisha kweli wewe, au wamekulea kama yai. Ndiyo maana hata kupika kwenyewe hujui, ukipiga maharage michuzi mimaji mimaji mama, maharage kwake, maji kwake, ukipika samaki wananuka shombo ng'eee, samaki wana upikaji wake, mtoto wa kike lazima utulize akili na mikono..."

Ilikuwa saa 12:00 asubuhi. Kama kawaida Havijawa walisubiri kaka yake adamke kwenda kazini akaenda kumsumbua wifi yake. Mlango ulifunguliwa kwa nguvu kiasi cha kumtisha mpaka Havijawa mwenyewe.

"Unasemaje wewe!?" Ilikuwa sauti kavu ya Sauda iliyochanganyikana na hasira.

Havijawa alilitambua hilo, akashangaa kuona kama wifi yake leo na yeye ameamka kisharishari.

"Unasemaje hiyo vipi? Unanitisha?"

"Siyo nakutisha, huyo kaka yako hataki mimi nimpikie chai alfajiri. Mimi nilikuwa tayari kufanya hivyo, lakini mwenyewe akaniambia ofisini kwake wanakunywa chai, kwa hiyo hapendi kunisumbua mkewe kuamka asubuhi asubuhi, akakataa hata kumpikia usiku na kumwekea kwenye chupa ili alfajiri aamke. Kama mimi naongopa njoo umuulize mwenyewe. Sitaki mimi kunisingizia uongo."

"Haya na kuzaa nako, maana mwaka unakatika huu hatuoni hata hamu ya kula embe mbichi!"

Hii ndiyo siku ambayo Sauda alikuwa akiisubiri kwa hamu. Alitaka kuufanyia kazi ushauri wa shoga yake Paulina na shoga ya huyo huyo wifi yake ambaye hakupenda tabia ya rafiki yake kumsumbua, kumsema na kumbugudhi mke wa kaka yake.

"Hivi wewe mwanamke, kipi ambacho mimi haswa nimekukosea?" Uulizaji ule na jinsi alivyokuwa siku hiyo ilionekana kabisa kuna kitu amedhamiria. Hata hivyo kwake haikuwa tatizo.

"Ahaa hukijui eeee."

**INAENDELEA JUMAPILI**




# SAUTI ZA BUSARA YAWASHA MOTO ZANZIBAR

TAMASHA la muziki la Sauti za busara linalofanyika Zanzibar kila mwaka, usiku wa jana limewasha moto baada ya Wasanii mbalimbali kuonyesha umahiri wao jukwaani na kuwapagawisha mashabiki wa muziki.

Katika usiku wa kwanza kundi la Dogo Fara kutoka Reunion lilifungua pazia kwa kupanda jukwaani na kuimba nyimbo zao ambazo zilionekana kuwarusha vilivyo wapenzi wa muziki.

Baada ya kushuka jukwaani, kiongozi wa kundi hilo, Masai amesema amefurahishwa na jinsi tamasha hilo lilivyoandaliwa na kutaja kama moja ya jukwaa bora barani Afrika.

"Nimefurahi kuona watu wa Zanzibar wakiwa wakarimu na kufurahia kazi yetu ya leo. Tumeona jinsi walivyotuunga mkono kwa kila tulipopanda jukwaani," Amesema Masai.

# SITI BAND LAPAGAWISHA NGOME KONGWE

KUNDI la Siti the band lenye makazi yake Zanzibar, wamewasha moto jukwaani baada ya muziki wao wenye mchanganyiko wa asili kuwakonga mashabiki waliokusanyika ndani ya ukumbi wa ngome kongwe.

Kundi hilo lenye mchanganyio wa wasanii kutoka visiwani humo na Tanzania Bara, limetumbuiza nyimbo zaidi ya nne zenye mahadhi ya makabila mbalimbali ya Tanzania na kuuweka katika muziki wa kisasa.

Akizungumza na gazeti hili mmoja wa wasanii wa kundi hilo aliyejitambulisha kwa jina la Jimmy, amesema kile walichoonyesha katika tamasha la sauti za Busara ni matokeo ya kujituma na ubunifu walioufanya kwa muda mrefu.

Amesema tamasha hilo limewafikisha mbali kutokana na kupata mialiko sehemu mbalimbali duniani baada ya kuonekana katika jukwaa hilo.

"Ni faraja kuona watu wanapokea vizuri kama ngoma ya bendi yenye asili ya Zanzibar.

Tunataka kufanya vizuri tunanufaika na jukwaa la sauti za burasa na kutupa nafasi ya kujulikana kimataifa kutokana na hapa tulipotoka."

Dogo Farah kutoka nchi ya Reunion Masai amesema amefurahishwa na tamasha la mwaka huu kwa kuwaona watu waliojitokeza.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FERNANDOED AITAKA BARCA

KIUNGO wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez, mwenye umri wa miaka 23 anataka kuondoka Chelsea na kujiunga na Barcelona licha ya mkataba wake na klabu ya Stamford Bridge kumalizika ifikapo mwaka 2032. **(Sport)**

### PALIHNHA ANUKIA BAYERN

BAYERN Munich wamemjumuisha mchezaji wa Fulham na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28 kwenye orodha yao ya kumnunua kiungo mpya msimu huu wa joto. **(Bild)**

### ADARABIONO SOKONI EPL

KLABU ya Liverpool inamfuatilia mlinzi wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26. **(90 min)**

### ROBINSON ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL pia wanafikiria kumnunua mlinzi wa Fulham na Marekani, Antonee Robinson, mwenye umri wa miaka 26, ili kumsaidia mlinzi wao wa kushoto wa Scotland, Andy Robertson (29). **(Fichajes)**

### KELLY AGOMBEWA ULAYA

MLINZI wa Bournemouth, Lloyd Kelly, mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuingia katika mpango wa kuhamia Liverpool au Tottenham Hotspur, huku AC Milan, Juventus na klabu kadhaa za Ujerumani pia vikimtaka raia huyo wa England ambaye anapatikana kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto. **(Football Insider)**

### ONANA ATAJWA BARCELONA

BARCELOANA imefanya mawasiliano na Everton kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo wa kati wa Ubelgiji, Amadou Onana, mwenye umri wa miaka 22, ambaye pia anaivutia Arsenal na Chelsea. **(Sport)**

### HARRISON MAMBO MAGUMU

MATUMAINI ya Everton kumsajili winga, Jack Harrison, mwenye umri wa miaka 27, kutoka Leeds United yamo shakani huku kukiwa na hali ya sitoafahamu kuhusu uwezekano wa kuchukua nafasi hiyo na mustakabali wao wa Ligi Kuu England. **(Football Insider)**

### AJAX, PSV VITANI

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott mwenye umri wa miaka 22 amezivutia Ajax na PSV Eindhoven baada ya msimu mzuri alioutumikia kwa mkopo katika klabu ya Excelsior Rotterdam. **(Wana 42)**

### GALLAGHER KUWEKWA SOKONI

CHELSEA itajaribu kusawazisha vitabu vyao msimu utakapomalizika kwa kumuuza kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 24 na nyota wengine mbalimbali. **(Football Insider)**

### CHELSEA, UNITED, PSG VITANI

CHELSEA, Manchester United na Paris St-Germain zinamfuatilia kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 26, huku kukiwa na sitofahamu kuhusu mustakabali wake Barcelona. **(Sport)**

### ARSENAL KUMTOA MARQUINHOS

KLABU ya Arsenal imekubali mkataba wa kumpeleka winga wa Brazil, Marquinhos, mwenye umri wa miaka 20 kwenda Fluminense kwa mkopo. **(Fabrizio Romano)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: HATUWEZI KUTWAA MATAJI MATATU

Kocha huyo afunguka hiyo ni 'hadithi ngumu' ambayo...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema ana asilimia 99.99 ya uhakika Manchester City haitarudia mafanikio ya kushinda mataji matatu msimu huu kama ilivyofanya katika uliopita.

City wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA msimu huu baada ya kubeba mataji yote matatu mwaka jana.

Watakuwa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu England, angalau kwa saa chache - kama jana wataifunga Everton.

Pia wana mechi za hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA raundi ya tano ijayo mwezi huu, lakini Guardiola amepunguza uwezekano wa timu yake kuwa timu ya kwanza ya England kushinda mataji matatu mfululizo.

„Hii ni hadithi, ni ngumu zaidi kuliko hiyo," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari. „Jaribu kuwashinda Everton na tutaona kitakachotokea. Tuna uwezekano wa asilimia 99.99 hatutashinda mataji matatu mfululizo kwa sababu kamwe, kamwe, kamwe, milele, milele, hajawahi mtu yeyote kufanya hivyo.

„Kama ilikuwa rahisi, timu nyingine (Manchester United wakati huo), ingefanya hivyo tena. Si rahisi.

"Kila kitu ni kigumu sana katika biashara hii, tulichokifanya siku za nyuma hakituhakikishii chochote, inabidi ufanye mambo yote tena kila baada ya siku tatu ili ukae pale hadi mwisho.

„Tunatumaini tutafika Machi na Aprili tukiwa na hisia sawa za kupigania mataji mwezi Mei. Hili ndilo lengo."

City wameimarishwa na kurejea kwa Kevin De Bruyne, Erling Haaland na John Stones na kuendeleza ushindi wao hadi michezo tisa kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya Brentford Jumatatu iliyopita.




# SALAH KUREJESHA KICHEKO LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ametoa kauli chanya kuhusu utimamu wa Mohamed Salah, akifichua mshambuliaji huyo anatazamia kurejea uwanjani wiki ijayo.

Salah alipata jeraha la msuli wa paja katikati ya Januari akiwa na Misri kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) na alitolewa nje kwa muda hadi mwisho wa Februari, akikabiliwa na kinyang'anyiro cha kuwa sawa kwa pambano la fainali la Kombe la Carabao dhidi ya Chelsea.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ameongeza ahueni yake hivi karibuni na ataanza mazoezi na Liverpool.

Akizungumza na waandishi wa habari, Klopp alifichua ratiba ya kupona kwa Salah.

"Tunatumaini anaweza kuwa sehemu ya mazoezi wiki ijayo, kwa hiyo lazima tuone, anapitia hatua zote," alisema Klopp kuhusu Salah.

"Lakini angalia, ni chanya. Ni wiki ijayo au wiki inayofuata, ukimuuliza ni wiki ijayo."

Liverpool itasafiri hadi kwenye Uwanja wa Gtech Community kumenyana na Brentford katika mechi ya Ligi Kuu England itakayochezwa Februari 17, mwaka huu na mchezo huo unaweza kuwa wa kwanza kwa Salah tangu arejee uwanjani.

Wekundu hao hawajashinda ugenini dhidi ya Nyuki hao tangu kupanda kwao Ligi Kuu England, sare ya 3-3 mnamo 2021/22 na kupoteza 3-1 msimu uliopita, ingawa walishinda 3-0 pale Anfield mapema kampeni hii.

Iwapo Salah hatarejea Brentford, atakuwa akitazama safari ya Luton Town kwenda Anfield mechi itakayofanyika Februari 21, siku nne kabla ya kukutana na Chelsea huko Wembley kwenye Kombe la Carabao.

Mechi ya mwisho ya Salah kwa Liverpool ilikuwa mwaka mpya katika ushindi wa 4-2 nyumbani dhidi ya Newcastle United.

Katika mechi saba ilizocheza Liverpool hadi sasa akiwa hayupo, Liverpool wameshinda tano, sare moja na kupoteza moja, huku msururu wao wa kutoshindwa ukiishia mikononi mwa wapinzani wao wa taji Arsenal, Jumapili iliyopita.

# Chelsea yamwania De Jong

**LONDON, England**

CHELSEA imetajwa kuwa moja ya klabu zinazomwania, Frenkie de Jong, ikiweka mezani ofa ya paundi milioni 85, baada ya kufahamu kiungo huyo tayari ameonyesha nia ya kuondoka Barcelona msimu wa joto.

Nyota huyo raia wa Uholanzi alionekana huenda akajiunga na Manchester United mwaka 2022 baada ya klabu hiyo ya England kutoa ofa ya pauni milioni 70 lakini De Jong aliamua kubakia kwa vigogo hao wa LaLiga.

Hata, hivyo baada ya kukumbana na majanga ya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara, kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, anatajwa ameamua kuweka wazi anahitaji kupata changamoto mpya, lakini pia sasa anahusishwa na kocha wa Red Devils, Erik ten Hag, ambaye alimkuza.




Kwa maana hiyo, inaelezwa huenda De Jong akawa na nafasi kubwa ya kujiunga na Manchester United.

Lakini Sport, limeandika The Blues wanahitaji kuongeza nguvu kusaka mchezaji namba sita na ndio sababu ya kuweka dau hilo la kumsajili nyota huyo na kujiunga na klabu hiyo ya Stamford Bridge.

Taarifa zinaeleza pia, De Jong, ambaye amebakisha miaka miwili katika mkataba wake na klabu hiyo ya Katalunya, pia anawindwa na vigogo wa Ufaransa, PSG.

De Jong anatajwa kuwa ni mmoja kati ya wachezaji wa Barcelona ambao wanalipwa kiasi kikubwa cha mshahara.

Chelsea tayari imeshatumia kiasi cha paundi milioni 280 katika kuimarisha idara yake ya kiungo katika kipindi cha miezi 12.

# Nyota Madrid amkataa Mbappe

**MADRID, Hispania**

GOLIKIPA wa Real Madrid, Andriy Lunin, amekiri afadhali kumchezesha Erling Haaland wa Manchester City kama mshambuliaji wa kati kuliko Kylian Mbappe wa Paris Saint-Germain.

Haaland na Mbappe wote wamehusishwa kwa kiasi kikubwa na kuhamia Madrid katika miaka ya hivi karibuni, ingawa hakuna hata mmoja ambaye amehamia Santiago Bernabeu.

Wakati uvumi ukiendelea kuvuma juu ya uhamisho wa siku zijazo, Lunin amechochea moto na jibu la uhakika katika maswali na majibu ya haraka na El Chiringuito.

Alipoulizwa kuchagua kati ya Haaland na Mbappe, Lunin alijibu: "Kama namba tisa, Erling Haaland."

Haaland amecheza kama namba tisa pekee katika maisha yake ya soka, wakati Mbappe amecheza katika nafasi mbalimbali kwenye mstari wa mbele, mara nyingi akicheza winga ya kushoto au chini katikati kama sehemu mbili za mbele.

90min iliripotiwa mapema wiki hii PSG ina orodha fupi ya walengwa - ikiwa ni pamoja na Marcus Rashford wa Manchester United, Victor Osimhen (Napoli) na Benjamin Sesko wa RB Leipzig - ikiwa Mbappe ataondoka msimu huu wa joto.

Mkataba wa Mbappe unamalizika Juni lakini kutokana na makubaliano magumu ya kisheria na PSG, klabu hiyo italazimika kurejesha hadi euro milioni 80 kama bonasi za uaminifu na mambo mengine iwapo ataondoka mwishoni mwa msimu.

Wakati huo huo, vyombo vya habari vya Hispania vimetangaza habari za kuhamia Madrid kwa Haaland, na kudokeza hana furaha kule England.

Hata hivyo, Pep Guardiola hivi majuzi alitoa changamoto kwa Madrid kuwapigia simu City na kuuliza kuhusu kupatikana kwa Haaland, akisema: "Hautakuwa uhamisho. Itatokea Erling atakapoamua kuongeza mkataba au la, wakati klabu itaamua kuongeza mkataba au la, wakati tuna ofa zinazowezekana kwake au la.

"Ikiwa mtu anamtaka Erling ni rahisi - piga simu. Pigia City na uulize. Hivyo ndivyo tunavyofanya tunapotaka kusajili mtu. Sio ngumu.

"Bila shaka inabidi uipuuze vyombo vya habari vinavyozungumza. Naijua hali halisi ya dunia hii. Hainisumbui hata kidogo, kwa vile wachezaji wanazingatia kile wanachopaswa kufanya, mengine sio muhimu."

# BENCHIKHA AKIRI AZAM FC ILIWANYIMA USINGIZI

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kugawana pointi na Azam FC, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema haikuwa mechi rahisi na sasa anarejea uwanjani kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa jijini, Mwanza juzi.

Benchikha aliliambia gazeti hili anahitaji kuona mastraika wake wanakuwa watulivu wanapokaribia lango la wapinzani.

Kocha huyo alisema haikuwa mechi ya rahisi kwa sababu wapinzani wao walikuwa bora lakini wachezaji wake walipambana na kufanikiwa kupata bao la kusawazisha dakika za lala salama.

"Mechi ilikuwa na ushindani mkubwa, Azam FC walicheza vizuri, wametupa mtihani mkubwa, tumeona mapungufu yetu na sasa tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi ikiwamo safu ya ushambuliaji, na hata ulinzi kutoruhusu bao katika mchezo ujao," alisema Benchikha.

Naye beki wa Simba, Shomari Kapombe, alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu kutokana na kuruhusu bao la mapema ingawa walifanikiwa kusawazisha na kuvuna alama moja .

"Mechi haikuwa rahisi kwetu , Azam FC wamekuwa wakikaba wote wanapopoteza mpira, tumeruhusu bao la mapema lakini tukafanikiwa kusawazisha, haikuwa bahati kwa sababu tulitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia," alisema Kapombe.

Kocha wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesikitika kukosa ushindi katika mchezo huo ambao alifahamu mapema Simba wanapenda kupiga mipira mirefu ambayo haikuwasaidia kutokana na mabeki wa kati walionao waliizuia.

„Tumekosa nafasi nyingi, tumecheza mpira kulingana na mipango yetu, tuliwaheshimu wapinzani, Simba wamecheza mipira mirefu lakini hawana ubora," alisema Dabo.




Viongozi wa Kamati ya Olimpiki Tanzania- TOC, (katikati) wakiwa na washiriki wa Semina ya Uongozi na Utawala kutoka mikoa mbalimbali nchini baada ya kuhitimu mafunzo yaliyofanyika katika Kituo cha OlympAfrica kilichoko Mkuza, Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: TOC**

# TOC yawanoa viongozi wanawake

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

KAMATI ya Olimpiki Tanzania (TOC), imewataka viongozi wa vyama vya michezo wanawake kwenda kuyatumia vyema mafunzo ya uongozi na utawala waliyopata ili kusaidia kuendeleza michezo wanayosimamia hapa nchini, imeelezwa.

Akizungumza wakati wa kufunga semina ya utawala na uongozi wa michezo iliyofanyika katika Kituo cha Olimpiki Afrika kilichoko Kibaha, Pwani, Rais wa TOC, Ghulum Rashid, alisema washiriki wanatakiwa kwenda kuonyesha kwa vitendo elimu waliyopata na kwa kufanya hivyo watafikia malengo ya taasisi wanazosimamia.

Ghulum alisema TOC inaamini washiriki hao watapeleka pia elimu ya uongozi na utawala waliyopata katika mikoa yao huku pia aliwapongeza washiriki wote kwa kuonyesha kiu ya kujifunza mambo mbalimbali.

„Mnatakiwa kuyapeleka mafunzo haya mnakotoka, nendeni mkayaonyeshe kwa vitendo, msiwe watu wa kukusanya vyeti," alisema kiongozi huyo.

Naye Makamu wa Rais wa TOC, Henry Tandau, alisema wajumbe waliyoshiriki semina hiyo wamepata mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwasaidia katika kutekeleza vyema majukumu yao ya kila siku.

Tandau alisema katika semina hiyo ya siku tano washiriki walipata elimu mbalimbali kuhusiana na uongozi katika michezo, kutafuta udhamini na namna ya kushirikiana na vyombo vya habari ili kuitangaza michezo yao.

## Nigeria, Ivory Coast fainali nzito AFCON

INATOKA UK. 24

nusu fainali dhidi ya Jamhuri ya Kidemkorasia ya Congo (DRC).

Sebastien Haller ataongoza tena safu ya ushambuliaji, lakini Nicolas Pepe, anaweza kuchukua nafasi ya Max Gradel kwenye winga ya kulia.

Ivory Coast wanatarajia kutumia mfumo wao wa 4-3-3, huku wachezaji wanaoweza kuanza ni Fofana; Aurier, Boly, Ndicka, Konan, Kessie, Seri, Fofana, Pepe, Haller na Adingra.

**UTABIRI**

Kasi ya Ivory Coast na faida ya nyumbani inawafanya kupendwa na wasio na upande wowote, lakini bado kuna pengo la kiwango kati yao na Nigeria.

Hakika ni uamuzi wa kichwa au moyo linapokuja suala la kuchagua mshindi katika fainali hii ya AFCON.

Na wachezaji kama Osimhen, Lookman na Moses Simon kwa Nigeria wanapaswa kuwa na uwezo wa kushinda fainali hii ikiwa watapata mambo ya msingi na kuchukua nafasi zao.

Nigeria inapewa nafasi ya kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Ivory Coast

## Yanga kuzikimbia Simba, Azam FC

INATOKA UK. 24

tucheze kwa tahadhari," alisema Ally.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema vita ya ubingwa imekuwa kali hivyo lazima wawe makini kila mechi wanayocheza kuhakikisha wanapata ushindi na kutimiza malengo yao ya kutetea ubingwa wao msimu huu.

„Muhimu ni kupambana na kutumbukiza mpira nyavuni ili kupata matokeo. Kila mechi kwetu tunaichukulia umuhimu mkubwa hivyo hata hii iliyo mbele yetu tunahitaji kupambana na kupata ushindi kama ilivyokuwa zingine zilizopita," alisema Gamondi.

Gamondi alisema wako tayari na mchezo huo ingawa amekiri utakuwa mgumu kutokana kawaida ya zilivyo mechi za mikoani.

„Mechi zinazochezwa nje ya Dar es Salaam hazijawahi kuwa rahisi kutokana na aina ya viwanja, lakini tumejiandaa na mechi hiyo, nadhani itakuwa mechi nzuri kwa sababu wachezaji wengi tulionao wanavifahamu viwanja hiyo, na tunataka tushinde ili kuweke pengo kubwa kwenye msimamo wa ligi," alisema Gamondi.

Kipa wa Yanga, Metacha Mnata aliliambia gazeti hili, wamejiandaa vyema licha ya kutopata muda wa kupumzika kutokana na kucheza mechi mfululizo.

„Kwa niaba ya wachezaji tumejiandaa vizuri, unajua mechi zipo karibu karibu sana muda wa kupumzika au wa kufanya mazoezi unakosekana," alisema Metacha.

# Michezo

Jumapili Februari 11, 2024

Nipashe


**Guardiola: Hatuwezi kutwaa mataji matatu** UKURASA 21





# NIGERIA, IVORY COAST FAINALI NZITO AFCON

## ●●● Ni mechi isiyotabirika kutokana na rekodi zilizopita huku wenyeji...

**ABIDJAN, Ivory Coast**

FAINALI ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) itafanyika leo kwa kushuhudia wenyeji, Ivory Coast wakimenyana na Nigeria katika mchezo unaotarajiwa kuwa mkali na wenye kusisimua.

Yamekuwa ni mashindano ambayo yatadumu kwa muda mrefu katika kumbukumbu, baada ya timu nyingi zilizopewa nafasi kubwa ya kushinda kutupwa nje kabla hata ya robo fainali.

Ivory Coast hakika wametinga fainali kwa hali ya kustaajabu zaidi, wakikaribia kuondolewa katika hatua ya makundi kabla ya kuachana na kocha wao na kutinga 16 bora.

Ushindi wao dhidi ya Senegal na Mali ulikuwa wa kishindo, ulishangaza na sasa wanakutana na Nigeria, timu ambayo iliwafunga bao 1-0 katika mchezo wa pili wa hatua ya makundi.

Super Eagles hao wamekuwa wa kuvutia sana wakati wa AFCON, lakini bado kuna hisia wana gia zaidi za kuongeza, bila kujali, wamebakiza mchezo mmoja tu kuunda historia.

**UNACHOPASWA KUJUA**

Mchezo wa Nigeria vs Ivory Coast utapigwa katika jiji la Abidjan kwenye Uwanja wa Alassane Ouattara kuanzia saa 5:00 usiku kwa saa za hapa Bongo.

Nigeria na Ivory Coast zimekutana mara tano katika mechi zilizopita za hivi karibuni.

Katika mechi hizo tano, Nigeria imeshinda mara tatu na Ivory Coast imeshinda mara mbili na hakukuwa na sare.

Mara ya mwisho Nigeria kukutana na Ivory Coast ilikuwa ni Janauri 18, mwaka huu kwenye hatua ya makundi ya AFCON hii na wakaibuka na ushindi wa bao 1-0.

Kiwango cha sasa kwenye michuano hiyo, Nigeria imeshinda mara tano, huku Ivory Coast ikishinda mara tatu na kupoteza mara mbili

NIGERIA

Nigeria huenda wakawa na kikosi cha kwanza kilichochoka zaidi kwa ajili ya fainali hii ya AFCON, baada ya kuzungusha kikosi chao kidogo sana kuliko Ivory Coast ambao walikuwa wakihaha kutafuta mshikamano mapema kwenye kinyang'anyiro hicho kwa kuwabadilisha wachezaji mara kwa mara.

Hakuna wasiwasi mpya wa majeruhi kutoka kwa kikosi cha Nigeria kinachonolewa na Kocha, Jose Peseiro.

Nigeria itawategemea zaidi, Victor Osimhen, pamoja na nyota mwenzake waanayecheza nae Ligi Kuu Italia, Serie A, Ademola Lookman.

Mfumo wa Nigeria unatarajiwa kuwa ni 3-4-2-1 na wachezaji watakaaonza ni Nwabali, Ajayi, Troost-Ekong, Bassey; Osayi-Samuel, Onyeka, Iwobi, Aina, Simon, Lookman na Osimhen.

**IVORY COAST**

Ni wachezaji wachache tu wa Ivory Coast kama Evan Ndicka, Franck Kessie na Seko Fofana ambao wamekuwa tegemeo kwenye timu hiyo.

Tembo hao wanaonekana kufika fainali wakiwa na ari kubwa na kwahiyo kuna sababu ndogo kwa kocha Emerse Fae kuanza kuhangaika na safu yake kutoka

INAENDELEA UK. 23

## Yanga kuzikimbia Simba, Azam FC

**Oliver Albert na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi, Yanga wanashuka kuwakabili wenyeji Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya huku presha yao ikishuka kutokana na sare waliyopata watani zao.

Yanga yenye pointi 37, imenufaika na sare ya bao 1-1 kati ya Simba na Azam, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, juzi, hivyo ushindi wa leo utawafanya kuendelea kuongoza kwa amani na utulivu zaidi ikiwa na tofauti ya pointi nane.

Tangu Yanga walipotoka suluhu na Kagera Sugar Februari 2 mwaka huu, mechi zao mbili ziliofuata walicheza katika presha kubwa ya kutafuta matokeo hivyo kujikuta wakipata ushindi dakika za mwishoni kutokana na kukabiliwa na mbio za ubingwa dhidi ya wapinzani wao wakubwa Simba na Azam.

Mechi dhidi ya Dodoma Jiji ilibidi wasubiri hadi dakika ya 85 kupata ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Mudathir Yahya ni kama ilivyokuwa katika mchezo uliopita walipoivaa Mashujaa FC, walishinda mabao 2-1 baada ya Mudathir kufunga goli la ushindi dakika 87.

Yanga itaikabili Prisons leo huku ikiwa na rekodi bora dhidi ya timu hiyo kwenye Uwanja wa Sokoine.

Katika mechi sita za karibuni ambazo timu hizo zimekutana katika Ligi Kuu kwenye uwanja huo, Yanga imeshinda michezo nne, zimetoka sare mechi moja huku Prisons ikishinda mchezo mmoja tu.

Mechi hizo sita ni tangu mwaka 2017 hadi sasa ambapo Prisons imewahi kuifunga Yanga mara moja tu na ilikuwa katika mchezo uliofanyika Mei 10, 2018 ambao maafande hao walishinda mabao 2-0.

Katika ushindi huo mchezaji pekee aliyebakia katika kikosi cha Prisons ni Jumanne Elifadhil pekee.

Kocha wa Prisons, Hamad Ally, amesema wanaiheshimu Yanga kwa sababu ni timu kubwa yenye wachezaji bora lakini wamejipanga kupambana nao.

„Tuko tayari kwa mchezo. Najua tunakutana na timu yenye wachezaji wenye akili kubwa ya kuamua matokeo muda wowote hivyo lazima

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >